## YALIYOMO:

Bali Wewe Usalipo – Mwongozo wa Kiongozi ……..………………...........02

Utangulizi ……………………………………..……..…………...…..10

Usiku wa Maombi ……………………………..…………….……......17

Changamoto za Kuwafikia watu walio nje ………….…..…………........19

Ahadi za Biblia Kudai kwenye Maombi ……………….…………..……23

Sherehe ya Siku ya Sabato ………………….……..……….………....33

Mahitaji ya Kuombea ya Kanisa la Kiulimwengu ……..………….........35

Siku ya 1 – Kaeni Ndani Yangu ………………………….………...………41

Siku ya 2 – Utufundishe Kuomba ……………..…….............................46

Siku ya 3 – Kuwa Dhahiri ……………………………..……..….............51

Siku ya 4 – Maombi Yasiyojibiwa (Na Imani) ………………….…........55

Siku ya 5 – Jina Lako Litukuzwe ……….............................................59

Siku ya 6 – Ufalme Wako Uje ……………..……................................64

Siku ya 7 – Mapenzi Yako Yatimizwe Hapa Duniani kama Huko Mbinguni ………………………….....................................................................68

Siku ya 8 – Utupe Leo Riziki Yetu ……....……………………………..73

Siku ya 9 – Utusamehe Deni Zetu kama Nasi Tuwasamehevyo Wadeni Wetu ……………..………..…..……...............................................77

Siku ya 10 – Usitutie Majaribuni ………………..…………...................81

**Bali Wewe Usalipo**

# Mwongozo wa Kiongozi

Karibu katika Siku Kumi za Maombi mwaka 2025! Tunaamini kuwa, katika maombi ndipo mahali uamsho unapozaliwa. Mungu ametenda miujiza mingi katika miaka iliyopita kadiri tulivyokuwa tukimtafuta katika maombi na kufunga. Roho Mtakatifu ameleta mabadiliko, ameamsha upya hisia za uinjilisti, makanisa yameamshwa na mahusiano yameponywa.

Je, sauti ya Mungu imekuwa ikikuita kufanya uamsho? Biblia imejaa ahadi nyingi kwa ajili yako:

"Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao" (*2 Nyakati 7:14*).

"Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote" (*Yeremia 29:13*).

"Na itakuwa ya kwamba mtu awaye yote atakayeliitia jina la Bwana ataponywa" (*Yoeli 2:32*).

"Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi" (*Yakobo 4:8*).

"Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami" (*Ufunuo 3:20*).

Popote ulipo katika maisha wakati huu wa sasa, Mungu yupo karibu na wewe zaidi kuliko unavyofikiria. Anataka kumwaga mibaraka Yake kwa familia yako, kwa kanisa lako, kwa jamii yako na kwa ulimwengu wako.

## Mambo ya Kawaida ya Maombi katika Siku Kumi za Maombi

### *Miongozo ya Maombi ya Kila Siku*

Tumetoa mwongozo wa maombi ya kila siku katika siku hizi kumi. Mwongozo wa kila siku husika unajumuisha aya ya Biblia, somo kwa ajili ya maombi, aya za Biblia za kutumia katika kuomba, mapendekezo ya maombi na mapendekezo ya nyimbo. Tunashauri kuwa ikiwezekana utoe nakala ya kurasa za miongozo ya kila siku ili kila mshiriki aweze kuwa na nakala yake apate kufuatisha katika ule muda wa maombi.

Makanisa ulimwenguni yataungana katika kuomba yakijikita katika mada ya siku husika. Ungana nao katika kuomba kupitia katika aya na mahitaji yaliyoletwa, lakini usihisi kwamba unapaswa kupitia kwa haraka katika orodha yote ya mahitaji ya maombi. Mnaweza kugawanyika katika vikundi vidogo na kila kikundi kikaombea sehemu ya orodha ya mahitaji yenu ya kuombea

Pia tumejumuisha ukurasa unaoitwa Maombi ya Kanisa la Kiulimwengu. Ni muhimu kuomba pamoja kwa ajili ya familia ya kanisa letu la kiulimwengu, lakini unaweza kutenga muda zaidi wa kuombea mahitaji ya sehemu mahalia ikiwa kundi lako linajumuisha wageni kutoka katika jamii husika. Omba kuhusu namna unavyoweza kuwakaribisha wageni kwa ubora zaidi na kuwafanya wajisikie kuwa ni sehemu ya kundi hilo.

Muda unaopendekezwa kwa ajili ya kila Kipengele cha Maombi

Fanya muda wenu wa maombi kuwa wa kawaida na rahisi kadiri iwezekanavyo ili kikundi chenu kiweze kuelekeza mawazo katika kuomba. Muda utakaotumika katika kila kipengele utatofautiana. Mwongozo ufuatao ni mapendekezo tu:

- **Ukaribisho na utangulizi** – dakika 2 hadi 5
- **Soma somo la maombi (mwongozo wa maombi wa kila siku) –** dakika 5

- **Kuomba Kupitia mafungu katika "Kuomba kwa Neno la Mungu" (mwongozo wa maombi wa kila siku)** – dakika 10 hadi 15
- **Kuombea mahitaji katika "Mapendekezo zaidi ya Maombi" (mwongozo wa maombi wa kila siku)** – dakika 20 hadi 30
- **Kushukuru kwa nyimbo na sifa** – dakika 5 – 10

***Kuombea Wengine***

Hamasisha kila mtu kuombea watu watano hadi saba ambao Mungu ameweka katika maisha yao. Wanaweza kuwa ndugu, marafiki, wafanyakazi wenza, majirani au watu wanaofahamiana nao. Wahamasishe kumwomba Roho Mtakatifu awaongoze katika kuchagua majina ya watu hao na kuhakikisha wanawafikia ndani ya siku hizi kumi za maombi. Unaweza kutoa kadi au vikaratasi ambavyo watu watatumia kuandika majina watakayokuwa wakiombea.

***Huduma za Sabato katika Kipindi cha Siku Kumi za Maombi***

Maombi na yalenge katika kitu mahususi na ni vyema kushiriki pamoja shuhuda mbali mbali za maombi yaliyojibiwa katika huduma siku ya Sabato kanisani Jumamosi zote mbili. Iweni wabunifu – kuna namna nyingi za kushiriki pamoja na familia ya kanisa mambo yanayotokea katika mikutano ya maombi ya kila siku.

***Sherehe ya Sabato ya Kuhitimisha***

Sabato ya mwisho inapaswa kutayarishwa kwa namna itakayokuwa ni muda wa furaha kuu kwa yale yote Mungu aliyotenda katika siku hizi kumi. Tenga muda wa kutosha kwa ajili ya shuhuda za maombi yaliyojibiwa, kwa ajili ya mafundisho ya kibiblia/mahubiri juu ya maombi, na kwa ajili ya nyimbo. Ongoza kusanyiko katika muda wa maombi ili kwamba hata wale ambao hawakuhudhuria mikutano ya kila siku, wapate uzoefu wa furaha ya kuomba pamoja na wengine. Tafadhali tazama mwongozo wa Sherehe za Sabato kwa mawazo zaidi.

***Kufuatilia kipindi hiki cha maombi ya siku kumi***

Omba ili kupata ufahamu jinsi Mungu anavyotaka kanisa au kikundi chako kuendeleza kile Alichoanzisha katika kipindi hiki cha Siku Kumi za Maombi. Pengine mtaendelea kukutana kila juma kwa ajili ya maombi. Au pengine Mungu anataka muanze huduma mpya ndani ya kanisa lenu au katika kuifikia jamii. Muwe tayari na kumfuata Mungu kule anapowaelekeza. Hakika mtashangazwa kadiri mnavyotembea pamoja Naye. Ukurasa kwa ajili ya Changamoto ya Kuwafikia Wengine umejaa mawazo ya huduma.

***Shuhuda***

Tafadhali shiriki visa vinavyoonesha jinsi Mungu alivyotendakazi katika Siku Kumi za Maombi! Visa vyako vitakuwa msaada na hamasa kwa wengine wengi. Shuhuda zinaweza kutumwa mtandaoni kwenye tovuti hii: www.tendaysofprayer.org.

## Vielekezi vya Muunganiko katika Maombi

***Kubalianeni***

Mtu anapoombea hitaji fulani kwa Mungu, hakikisha kuwa wengine pia wanaombea hitaji hilo hilo na kukubaliana – kufanya hivi kuna nguvu! Usifikiri kwamba kwa sababu mtu mmoja ameomba kuhusu hitaji hilo, hakuna haja ya mwingine kuliombea. “Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lo lote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni” (Mathayo 18:19). Inatia moyo kiasi gani kuinuliwa katika maombi!

***Kudai Ahadi za Mungu***

Hamasisha kikundi kudai ahadi za Mungu kadiri wanavyoomba. Ni rahisi sana kujielekeza katika matatizo yetu. Lakini tunapodai ahadi za Mungu, tunaongeza imani yetu na kujikumbusha kwamba hakuna kinachoshindikana kwa Mungu.

Ahadi hizo hutusaidia kuondoa macho yetu kwenye madhaifu yetu na magumu tunayokabiliana nayo, hivyo kuyaelekeza kwa Yesu. Tunaweza kupata ahadi za Biblia za kudai kwa kila udhaifu na kila pambano. Himiza watu kutafuta ahadi nyingi zaidi kadiri iwezekanavyo na kuziandika ili waweze kuzidai katika maombi wakati ujao.

***Kufunga***

Alika wale wanaoungana nawe katika Siku Kumi za Maombi kufikiria aina ya kufunga watakayoshiriki, kwa mfano kufunga na kuacha kutazama televisheni, kuacha kusikiliza muziki wa kidunia, kuacha kutazama filamu, kuacha kuingia mtandaoni, kuacha kula vitu vitamu vitamu kama vile pipi au aina nyingine za vyakula ambavyo ni vigumu kumeng'enywa. Tumia muda wa ziada katika kuomba na kujifunza Biblia, ukimwomba Mungu akusaidie wewe na kusanyiko lako kudumu kikamilifu zaidi katika Kristo. Kwa kuchagua mlo mwepesi, tunaruhusu akili zetu kuwa sikivu zaidi kwa sauti ya Roho Mtakatifu.

***Roho Mtakatifu***

Hakikisha unamwomba Roho Mtakatifu akuoneshe jambo la kuombea katika maisha ya mtu fulani au katika hali fulani. Biblia inatuambia kwamba hatufahamu tuombe nini, na kwamba Roho Mtakatifu ndiye anayetuombea.

"Hatupaswi kuomba tu kwa jina la Kristo, bali kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu. Hii huelezea maana halisi tunaposema kuwa Roho 'hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa' (Warumi 8:26). Mungu hufurahia kujibu ombi kama hilo. Tunapoomba kwa dhati na kwa nguvu tunaomba kwa jina la Kristo, katika nguvu hiyo kuna ahadi kutoka kwa Mungu kwamba anakaribia kujibu maombi yetu kama tunavyosoma kuwa, 'Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu' (Waefeso 3:20)" (Christ Object Lessons, uk. 147, msisitizo umeongezewa).

***Kutunza Taarifa ya Maombi***

Kutunza daftari la kumbukumbu ya maombi kwenye kipindi chote cha Siku Kumi za Maombi kunaweza kuwa njia bora ya washiriki kuhifadhi moyoni wazo kuu la maombi ya kila siku, kufanya maagano thabiti na Mungu na kutambua mibaraka Yake kwao. Kuorodhesha maombi yetu na kutunza kumbukumbu ya majibu ya Mungu ni njia iliyothibitishwa na ya kutia moyo.

Ikiwa utapenda, unaweza kutenga muda pale mnapokutanika kwa ajili ya maombi, ili watu wapate kuandika mwitikio wao kwa Mungu kwenye shajara zao binafsi za maombi. Au unaweza kutunza shajara ya kikundi cha maombi na majibu yake – linaweza kuwa ni daftari au bango kubwa, au unaweza kutunza mtandaoni. Inafurahisha na pia inajenga imani unapotazama nyuma na kuona jinsi Mungu alivyojibu maombi!

***Kicho***

Himiza na kujenga mtazamo wa kicho na unyenyekevu. Tunakaribia chumba chenye kiti cha enzi cha Mfalme wa ulimwengu. Hebu tusitumie muda huu wa maombi vibaya kwa mkao na kwa mwenendo wetu usiofaa na hata katika mazungumzo yetu. Hata hivyo, siyo lazima kila mmoja apige magoti muda wote. Unahitaji watu wawe huru kwa saa moja, hivyo wahamasishe watu kupiga magoti au kukaa au kusimama kadiri Mungu atakavyokuongoza na kwa namna wanavyokuwa huru zaidi.

***Maombi ya Sentensi***

Maombi yanapaswa kuwa mafupi na yaelekezwe moja kwa moja kwenye hitaji. Kufanya hivi kutawapatia wengine pia fursa ya kuomba. Jaribu kufupisha maombi yako yawe ni ya sentensi chache. Kila mmoja anaweza kuomba mara kadhaa. Maombi mafupi yatafanya kipindi cha maombi kiwe cha kufurahisha na siyo cha kuchosha na hivyo kumruhusu Roho Mtakatifu aguse kundi zima akiwaonesha namna ya kuomba.

Siyo lazima kuanza na kumaliza kwa ombi fupi la sentensi kwa maneno kama “Mungu wetu mpendwa” na “Amina.” Ni mawasiliano endelevu na Mungu.

***Ukimya***

Wewe kama kiongozi, usitawale kipindi cha maombi. Lengo kubwa ni kuwawezesha wengine kuomba. Kipindi cha ukimya kina thamani kubwa ajabu, kwani humpa Mungu muda wa kuzungumza na mioyo yetu. Mruhusu Roho Mtakatifu afanye kazi kwa kumpa kila mmoja muda wa kutosha wa kuomba.

***Kuimba***

Nyimbo za hapa na pale kutoka kwa vikundi, zikiunganishwa kwenye maombi, huongeza uzuri katika mkutano wa maombi. Nyimbo zilizopendekezwa zimeorodheshwa mwisho wa kila ukurasa wa wazo la siku. Si lazima kutumia nyimbo zote – haya ni mapendekezo tu. Kuimba pia ni njia nzuri ya kuhama kutoka kwenye kipindi kimoja kwenda kwenye kipindi kingine.

***Kukusanya Mahitaji ya Kuombea***

Usiulizie wala kukusanya mahitaji ya kuombea kutoka kwenye kikundi. Badala yake, waambie watu wataje mahitaji yao wakati wanapoomba na kuwahimiza wengine kujiunga wakikubaliana nayo kwa kuungana katika maombi kimya kimya. Sababu kubwa ni Muda! Kuzungumza kuhusu mahitaji ya kila mmoja kunaweza kutumia muda mwingi wa maombi. Shetani anafurahi akiweza kutudumisha katika kuzungumzia tatizo badala ya kuomba kwa ajili ya tatizo hilo. Wanakikundi wanaweza kuanza kushauriana na kupendekeza ufumbuzi. Uweza unatoka kwa Mungu! Kadiri tunavyoongeza maombi, ndivyo anavyoachia uweza Wake.

***Muda Wako wa Kila Siku***

Ni wa muhimu sana! Hakikisha wewe kama kiongozi unatumia muda wako mwingi miguuni pa Yesu, ukizungumza Naye na kusoma Neno Lake. Ikiwa utafanya kumfahamu Mungu kuwa kipaumbele katika Maisha yako, utafunguliwa uzoefu ulio mzuri na wa ajabu. “Kutoka katika sehemu ya siri ya maombi ilitoka Nguvu ya ajabu iliyotikisa dunia na kuleta Matengenezo Makuu. Hapo, kwa utulivu mtakatifu, watumishi wa Bwana waliweka miguu yao katika mwamba wa ahadi zake” (The Great Controversy, uk. 210). Kiongozi anapoomba, Mungu hushughulika na mioyo!

## Utangulizi

Karibu katika Siku Kumi za Maombi 2025! Tunaamini kuwa, katika maombi ndipo mahali uamsho unapozaliwa. Mungu ametenda miujiza mingi katika miaka iliyopita kadiri tulivyokuwa tukimtafuta kwa kuomba na kufunga. Roho Mtakatifu amewezesha uamsho, mabadiliko, hisia za uinjilisti zilizojengwa upya, makanisa yaliyoamshwa na mahusiano yaliyoponywa. Hapa kuna baadhi ya shuhuda katika miaka iliyopita:

*"Wakati wa Siku Kumi za Maombi za mwaka huu, Mwenyezi Mungu alifanya miujiza mingi ya kutisha…. Katika eneo jirani na moja ya makanisa yetu, kumekuwa hakuna umeme kwa karibu miaka miwili…. Kwa hiyo wakati wa Siku Kumi za Maombi zilizopita, mchungaji wa kanisa alivuviwa kulitaka kanisa kuomba kila siku asubuhi ili umeme urejeshwe. Kwa utukufu wa Mungu maombi hayo yameendelea kujibiwa."* **(P. C. O.)**

*"Wakati wa Siku Kumi za Maombi, kulikuwa na kujitoa upya, hamasa mpya, bidii mpya, uaminifu mpya miongoni mwa kusanyiko. Binafsi, niliona kwamba hutupatia kuumbwa upya, na hata zaidi sana wakati wa hitimisho kwa mkesha wa maombi ya usiku yenye mafanikio mazuri! Tunahitaji vipindi hivyo vya pekee vinavyotuleta karibu na miguu ya Yesu vingi zaidi."* **(E. A.)**

*"Kujitoa kwangu kusoma Maandiko na kutumia muda katika maombi hakukuwa kwa dhati hivyo. Baada ya Siku Kumi za Maombi nilibadilisha sana mtazamo wangu kuhusu maombi. Nilianza kutumia muda mwingi katika maombi, nikimsifu Mungu, nikiomba kwa ajili ya wengine, na kuyasoma Maandiko. Nilikuwa na shinikizo la juu la damu, lakini limepungua tangu wakati huo. Shukrani zangu zote ni kwa Mwenyezi Mungu."* **(H. R.)**

*"Wakati wa Siku Kumi za Maombi, kila mtu alimwombea dada ambaye alikuwa na usaili kwa ajili ya ajira. Aliajiriwa—katika kazi ambayo ilimhitaji mtu aliyekuwa na sifa za juu mno, lakini alipewa*

*yeye. Tunashangazwa na kile ambacho Mungu anaweza kukifanya, baada ya miaka mingi ya mahangaiko na kungojea. Je! Ni mara ngapi tumeomba? Hatuwezi kukumbuka idadi. Ninataka kuwatia moyo nyinyi nyote tuendelee kuomba kwa sababu maombi yetu hayatakuwa ya bure tukiamini."* **(L. B.)**

Je, sauti ya Mungu imekuwa ikikuita katika uamsho? Biblia imejaa ahadi kwaajili yako:

"Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao" (*2 Nyakati 7:14*).

"Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote" (*Yeremia 29:13*).

"Na itakuwa ya kwamba mtu awaye yote atakayeliita jina la Bwana ataponywa" (*Yoeli 2:32*).

"Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi" (*Yakobo 4:8*).

"Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami" (*Ufunuo 3:20*).

Popote ulipo katika maisha sasa, Mungu yupo karibu zaidi kuliko unavyofikiri. Anataka kumwaga mibaraka Yake kwa familia yako, kanisa lako, jamii yako na kwa ulimwengu wako!

**Mada yetu ya Maombi: Bali Wewe Usalipo ...**

Mwaka huu masomo yetu ya kila siku yaliandaliwa na Dr. Pavel Goia, mhariri wa gazeti la *Ministry*. Anatumia visa kutoka katika huduma yake mwenyewe ili kuchanganua Sala ya Bwana na mafundisho mengine ya Yesu. Fuatana naye anapofunua maana ya kina zaidi na umuhimu wa

kiroho wa aya zinazojulikana. Inamaanisha nini “kulitukuza” jina la Mungu? Je! Ufalme wa Mungu unaonekanaje hapa ulimwenguni? Je! Ni kwa jinsi gani kuwasamehe wengine kunabadilisha mahusiano yetu na Mungu? Na je! Mungu anaweza kuwatia watu majaribuni?

Huenda umekuwa ukiomba kwa maisha yote au siku chache tu, masomo haya yaliyojaa shuhuda (visa) yataamsha hisia zako za hitaji na shauku ya kukutana na Yesu kwenye magoti yako kila siku. Soma kwa uangalifu na uwe na Biblia yako karibu. Na kama inawezekana, tafuta kikundi cha waumini ili mwombe pamoja wakati wa siku hizi kumi. Wanapokusanyika wawili au watatu katika jina la Yesu, miujiza inatokea!

**Mwongozo Unaopendekezwa Wakati wa Maombi**

- Jitahidi kufanya maombi yawe mafupi – sentensi moja au mbili zilizojengeka katika mada husika. Kisha wape nafasi wengine. Unaweza kuomba mara nyingi kadiri unavyojisikia, kwa namna ile ile unayozungumza katika mazungumzo.
- Usitishwe na ukimya, kwani ukimya unampatia kila mmoja muda wa kumsikiliza Roho Mtakatifu.
- Kuimba nyimbo pamoja kadiri Roho Mtakatifu atakavyowaongoza ni mbaraka mkubwa. Hamhitaji kinanda ili kuwaongoza; kuimba bila ala ya mziki ni sawa pia.
- Badala ya kutumia muda wa thamani wa maombi ukizungumza kuhusu mahitaji yako ya kuombea, ni vyema uyaombee tu. Kisha wengine pia wanaweza kuombea mahitaji yako na kudai ahadi kwa ajili ya mahitaji yako.

**Kudai Ahadi**

Ni fadhila kwetu kudai ahadi za Mungu katika maombi yetu. Maagizo yote ya Mungu na mashauri yake pia ni ahadi. Hawezi kudai kutoka kwetu jambo fulani ambalo hatuwezi kufanya kwa uweza Wake.

Tunapoomba, ni rahisi kujielekeza katika mahitaji yetu, magumu yetu, changamoto zetu – na hasa kulalamika na kulaumu katika maombi kuhusu hali tuliyo nayo. Hili si kusudi la maombi. Kusudi kubwa la maombi ni kuimarisha imani yetu. Ndiyo maana tunakuhimiza kudai ahadi za Mungu katika muda wako wa maombi. Hamisha macho yako kutoka katika mahitaji yako na changamoto zako na kuyaelekeza kwa Yesu Kristo. Ni kwa kumwangalia Yeye pekee ndipo tunapobadilishwa na kuchukua sura Yake.

Ellen White anatutia nguvu kwamba: "Kila ahadi katika Neno la Mungu ni kwa ajili yetu. Katika maombi yako, wasilisha neno lililoahidiwa la Yehova udai kwa imani ahadi Zake. Neno Lake linatupatia uhakika kwamba ukiomba kwa imani, utapokea mibaraka yote ya kiroho. Endelea kuomba nawe utapata zaidi ya yale uyaombayo au uyawazayo." (*In Heavenly Places, uk. 71*).

Ni kwa namna gani unaweza kudai ahadi hizo za Mungu? Kwa mfano, unapoomba kwa ajili ya amani, unaweza kudai kupitia Yohana 14:27 na kusema kuwa, "Bwana umetuambia katika Maandiko Yako kwamba 'Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga.' Ninakuomba unipatie amani uliyoahidi kutuachia." Kisha mshukuru Bwana kwamba atakupatia hiyo amani hata kama haujisikii kuwa na amani wakati huo.

**Kufunga**

Tunakuhamasisha kufanya Mfungo kama ule wa Danieli katika Siku hizi Kumi. Kuanza mwaka kwa maombi ya kufunga ni njia bora ya kuweka wakfu maisha yetu kwa Mungu kwa mwaka unaoanza. Ellen White anatuambia kuwa, "Sasa na kuendelea hata mwisho wa wakati watu wa Mungu wanapaswa kuwa na bidii zaidi, kuwa macho zaidi, kutokuamini hekima yao wenyewe, lakini kuamini hekima ya kiongozi wao, ambaye ni Yesu. Wanapaswa kutenga siku kwa ajili ya kufunga na kuomba. Kujitenga kabisa na chakula kunaweza kusiwe lazima, lakini wanapaswa kula vyakula rahisi zaidi kwa kujinyima" (*Counsels on Diet and Foods, uk. 188, 189*).

Tunafahamu kuhusu Danieli, aliyekula matunda na mbogamboga kwa siku kumi. Sisi pia tunakuhamasisha kuwa na mlo rahisi sana katika siku hizi kumi. Kama tunataka akili zilizo wazi zaidi ili kuisikia sauti ya Mungu, na kama tunataka kuwa karibu zaidi na Mungu, tunahitaji kuhakikisha kwamba chakula chetu hakiwi kikwazo.

Kufunga si kujitenga tu na chakula. Tunakuhamasisha pia kufunga kutazama televisheni, filamu, michezo ya kompyuta na hata Facebook na YouTube. Wakati mwingine vitu visivyo vibaya, kama Facebook na YouTube, huweza kutuchukulia muda mwingi sana. Weka kando kila kinachowezekana ili uwe na muda mwingi wa kukaa na Bwana.

Kufunga sio namna ya haraka ya kupata mibaraka kutoka kwa Mungu. Kufunga ni kujinyenyekeza wenyewe ili kwamba Mungu aweze kufanya kazi ndani yetu na kupitia kwetu. Hebu na tusogee karibu Naye kupitia maombi ya kufunga, Naye atasogea karibu zaidi nasi.

**Roho Mtakatifu**

Hakikisha unamwomba Roho Mtakatifu akuoneshe unachopaswa kuombea katika maisha ya mtu fulani, au katika hali fulani. Biblia inatuambia kwamba hatujui tuombee nini na kwamba Roho Mtakatifu ndiye anayetuombea.

“Hatupaswi kuomba tu kwa jina la Kristo, lakini kwa msukumo wa Roho Mtakatifu. Hii huelezea maana ya maneno kwamba Roho “hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa” (Warumi 8:26). Ombi kama hilo Mungu hufurahia kulijibu. Tunapoomba kwa dhati na kwa nguvu tunaomba kwa jina la Kristo, katika nguvu hiyo kuna ahadi kutoka kwa Mungu kwamba anakaribia kujibu maombi yetu ‘zaidi ya tuyaombayo au tuyawazayo’—Waefeso 3:20” (*Christ Object Lessons, uk. 147*).

**Imani**

Tunasoma katika Roho ya Unabii kwamba “maombi na imani vitafanya kile ambacho hakuna nguvu duniani inayoweza kufanya” (*The Ministry*

*of Healing, uk. 509*). Pia tunaambiwa kwamba "ahadi yoyote Aliyoahidi, tunaweza kuiomba; kisha tunapaswa kuamini kwamba tumeipokea, na kurudisha shukrani kwa Mungu kwamba tumepokea" (*Education, uk. 258*). Hivyo jenga tabia ya kumshukuru Mungu kwa imani kabla, kwa kile atakachotenda na namna atakavyojibu maombi yako.

**Ombea Wengine**

Katika siku hizi kumi tunakuhimiza kuombea watu ambao Mungu amewaweka katika maisha yako kwa namna ya pekee. Chagua watu watano hadi saba – wanaweza kuwa ndugu, marafiki, wafanyakazi wenzako, majirani au hata watu unaowafahamu tu. Tenga muda kumwuliza Mungu kuwa, angependa umwombee nani. Mwombe pia akupatie mzigo halisi wa watu hawa. Andika majina yao kwenye karatasi na uitunze sehemu salama, kama kwenye Biblia yako. Utashangazwa namna Mungu anavyofanya kazi katika kujibu maombi yako!

**Changamoto ya Kuwafikia Watu walio Nje ndani ya Siku Kumi za Maombi**

Yesu hatuiti kwa ajili ya kuomba tu bali anatuita ili pia, kuhudumia mahitaji ya wale wanaotuzunguka. "Kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia" *(Mathayo 25:35, 36)*.

Katika kitabu cha *Huduma ya Uponyaji (The Ministry of Healing)* tunasoma kuwa, "Tunapaswa kuishi maisha yenye sura mbili – maisha ya mawazo na matendo, na maisha ya maombi ya kimya na kazi inayofanywa kwa juhudi" (*uk. 512*). Tumepokea upendo mwingi sana kutoka kwa Mwokozi wetu; na tunayo fursa ya kushiriki upendo huo na marafiki, majirani, hata watu tusiowafahamu wenye uhitaji.

Mwulize Mungu katika maombi namna bora ya kuwafikia wengine

katika Siku hizi Kumi za Maombi. Unapokuwa ukifanya kazi ya kupanga kila kitu, epuka kuruhusu shughuli hizo kukufanya ushindwe kuomba. "Jitihada binafsi kwa ajili ya wengine zinapaswa kwanza kutanguliwa na maombi mengi ya faragha; kwani hekima kubwa inahitajika ili kuelewa sayansi ya kuokoa roho. Kabla ya kuwasiliana na watu, wasiliana na Kristo. Pata maandalizi ya kuhudumia watu kutoka katika kiti cha enzi cha neema ya kimbingu." (*Prayer, uk. 313*).

Katika nyenzo za Siku Kumi za Maombi mtandaoni, utapata nyaraka iliyojaa mapendekezo mengi ya kuwafikia wengine. Yesu anakualika kuwa mikono na miguu Yake kwa ulimwengu wenye uhitaji!

**Kuhusu Mwandishi**

Pavel Goia, DMin, ni mchungaji aliyewekewa mikono, mnenaji wa hadhara na mhariri. Alianza kazi yake ya uchungaji katika nchi yake ya Romania. Pavel na mke wake mpendwa, Daniela, walihamia Marekani pamoja na vijana wao wawili ili kuendeleza elimu ya Pavel katika huduma ya kichungaji. Alijisikia furaha  kuwa mchungaji wa makanisa kadhaa huko Romania na Marekani na amezunguka ulimwengu akizungumza juu ya maombi na mada zingine. Alikuwa mhusika wa kitabu kimoja, *One Miracle After Another: The Pavel Goia Story* na ni mwandishi wa makala nyingi na kitabu kiitwacho, *In the Spirit and Power*. Kwa sasa Pavel ni katibu wa wachungaji msaidizi wa Konferensi Kuu ya Waadventista wa Sabato na mhariri mkuu wa *Ministry*, Jarida la Kimataifa la Wachungaji. Anapenda kutumia wakati mwingi iwezekanavyo pamoja na mke wake mpendwa Daniela, vijana wao wawili, wajukuu wanne na mbwa wake mwadilifu.

Masomo haya yameandaliwa na Chama cha Wachungaji,

Konferensi Kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato.

Isipokuwa imeelezwa, nukuu zote zinatoka katika toleo la Biblia la

"Swahili Union Bible" © 1997

# USIKU WA MAOMBI:

Fikiria kuandaa huduma ya maombi ya usiku mzima kama sehemu ya Siku Kumi za Maombi. Kwa mfano, unaweza kuanza saa 12 jioni na kumaliza saa 12 asubuhi. Chagua ratiba itakayofaa kwa kundi lako.

***Kwa nini kuwa na Usiku wa Maombi?***

Hakuna chochote "kitakatifu" katika kukaa macho huku ukiomba usiku kucha. Hata hivyo, ni kweli kwamba usiku unaweza kuwa ni wakati wa pekee ambao watu hawana mambo mengi ya kufanya au kuwa katika hali ya haraka. Tunaamini kwamba lengo lako halipaswi kuwa kukaa macho usiku kucha, bali ni kuomba sana kadiri inavyohitajika hadi utakapokuwa umeombea vitu vyote unavyohisi kwamba Mungu anataka uviombee.

Tunapendekeza kwamba baadhi ya watu waongoze usiku huo. Hakikisha kunakuwa na mapumziko. Kama kiongozi, unaweza kuona hali ilivyo na kufahamu wakati mapumziko yanapohitajika na wakati utakapoona inafaa kuhamia katika kipengele kinachofuata cha maombi. Unaweza pia kuingiza usomaji wa aya za  Biblia katika muda wako wa maombi. Unaweza kufanya mambo yote yaliyopendekezwa au baadhi yake, inategemea kile kilicho bora kwa kikundi chako. Kuwa huru kubadilisha mtiririko kadiri utakavyoona inafaa.

**Mapendekezo ya Mpangilio wa Usiku wa Maombi**

- ***Anza kwa kipindi cha sifa***. Msifu Mungu katika maombi yako na pia kupitia nyimbo.

- ***Tumia muda kwa ajili ya kuungama***, ukihakikisha kwamba hakuna kinachomzuia Mungu kusikia maombi yako. Wapatie watu muda wa maungamo binafsi na weka muda wa kuungama kwa pamoja. Hamasisha watu kuungama dhambi zao binafsi wakiwa peke yao na kuungama dhambi za wazi kwa uwazi. Katika Danieli 9:1-19 tunasoma kumhusu Danieli, aliyeomba na kuungama kwa wazi dhambi za watu wa Mungu.

- ***Ombea mahitaji ya watu walio katika mkutano huo wa maombi***. Watu wengi wanaumia au wana uhitaji wa maombi, au wanamfahamu mtu mwenye uhitaji wa maombi. Tengeneza duara, weka kiti katikat, na alika wale wenye maombi maalum waje mmoja baada ya mwingine na kushiriki maombi yao. Kisha kusanyikeni kumzunguka mtu huyu na waruhusu watu wawili au watatu kuomba kwa ajili ya mahitaji mahususi ya mtu huyo na kudai ahadi za Mungu.

- ***Gawa kikundi katika vikundi viwili vidogo.*** Waruhusu wanawake kuomba katika chumba kimoja (wakiwa na kiongozi wa kike) na wanaume katika chumba kingine (wakiwa na kiongozi wa kiume). Mahitaji mengi binafsi hayawezi na hayapaswi kushirikishwa na kila mtu. Ni rahisi zaidi kushiriki pamoja na wale wa jinsia moja.

- ***Baada ya kurudi pamoja, ombea mahitaji ya jamii na kanisa lenu.*** Pia tumia muda kwa ajili ya **maombi ya kanisa la ulimwengu** (yaliyoorodheshwa katika ukurasa wa maombi ya kanisa la kiulimwengu). Sio lazima kumaliza orodha nzima ya maombi, kwa hiyo usiharakishe ukiwa na hisia za kutaka kumaliza orodha yote. Unaweza kugawa maombi katika vikundi vidogo na kuwapatia kila kikundi sehemu ya orodha hiyo.

- ***Ombea orodha ya watu watano hadi saba*** uliokuwa ukiwaombea katika siku hizi kumi

- ***Chagua aya ya Biblia na kuombea.***

- ***Funga muda wa maombi kwa kipindi kingine cha kusifu na kushukuru.***

## Changamoto za Kuwafikia watu walio nje

## Ndani ya Siku Kumi za Maombi

Yesu hatuiti kwa ajili ya kuomba tu bali anatuita pia ili kuhudumia mahitaji ya wale wanaotuzunguka. “Kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia” (*Mathayo 25:35, 36*).

Katika kitabu cha *Huduma ya Uponyaji (The Ministry of Healing)* tunasoma kuwa, “Tunapaswa kuishi maisha yenye sura mbili – maisha ya mawazo na matendo, na maisha ya maombi ya kimya na kazi inayofanywa kwa juhudi” (*uk. 512*). Tumepokea upendo mwingi sana kutoka kwa Mwokozi wetu; na tunayo fursa ya kushiriki upendo huo na marafiki, majirani, hata watu tusiowafahamu wenye uhitaji.

Mwulize Mungu katika maombi namna bora ya kuwafikia wengine katika Siku hizi Kumi za Maombi. Unapokuwa ukifanya kazi ya kupanga kila kitu, epuka kuruhusu shughuli hizo kukufanya ushindwe kuomba. “Jitihada binafsi kwa ajili ya wengine zinapaswa kwanza kutanguliwa na maombi mengi ya faragha; kwani hekima kubwa inahitajika ili kuelewa sayansi ya kuokoa roho. Kabla ya kuwasiliana na watu, wasiliana na Kristo. Pata maandalizi ya kuhudumia watu kutoka katika kiti cha enzi cha neema ya kimbingu” (*Prayers, uk. 313*).

Hapa kuna baadhi ya njia unazoweza kutumia kusaidia wengine. Chagua njia yoyote utakayoona inakidhi mahitaji ya wale unaokwenda kuwahudumia na jisikie huru kuongeza mawazo yako.

- Mpikie mgonjwa chakula.
- Mkaribishe jirani/mfanyakazi mwenzako kwenye kusanyiko la kijamii.

- Mpatie chakula mtu asiye na makazi.
- Tafuta mzee mmoja. Mtembelee kila siku na umsaidie kazi, kama vile kumnunulia mahitaji, kumpikia au kumsaidia kazi za bustani n.k.
- Oka mkate na ushiriki huo mkate na jirani.
- Saidia kwenye miradi katika maeneo yanayokuzunguka.
- Jitolee kukaa na mgonjwa au mtu asiyejiweza ili wale wanaomhudumia waweze kufanya shughuli zingine.
- Jitambulishe kwa jirani mpya aliyehamia maeneo yenu na kumpelekea chakula. Mfanye ajisikie kukaribishwa katika maeneo hayo.
- Nunua mahitaji ya jikoni na upelekee familia yenye uhitaji.
- Toa msaada miwani yako ya zamani.
- Jitolee kutoa masomo ya Biblia
- Tembelea sehemu za kutunzia watu wenye uhitaji na kuwafariji.
- Mpatie mwanafunzi fedha ya “chakula.”
- Kusanya nguo kwa ajili ya wahitaji. Unaweza kuanzisha kabati la nguo kanisani kwako kwa ajili ya kushirki na wale walio na uhitaji.
- Toa msaada wa kompyuta yako au vifaa vingine vya kielektroniki usivyotumia.
- Toa msaada gari lako lililotumika.
- Andaa “Tamasha la Kupima Afya.”
- Tuma kadi kwa mtu aliyefungiwa ndani.

- Andaa mfululizo wa mambo ya uinjilisti.
- Mpatie mtu kitabu unachodhani angekipenda.
- Wapigie simu jirani zako na kuwajulia hali.
- Gawa vijarida na vijuzuu kwa watu. Vinapatiakana kwenye tovuti ifuatayo hapa: www.glowonline.org/glow
- Mwalike mtu kumpokea Yesu.
- Endesha darasa la mapishi.
- Fanya "Mradi wa machapisho 28." Katika Juma la kwanza, gawa kitabu kimoja. Juma la pili, gawa vitabu viwili. Juma la tatu, gawa vitabu vitatu. Endelea hadi utakapogawa vitabu vyote 28.
- Mpelekee chakula mtu aliyepoteza (aliyefiwa na) mpendwa wake.
- Mtembelee mtu hospitali ili kumtia moyo au kumsaidia kwa namna moja au nyingine.
- Msomee mzee kitabu.
- Tembelea makazi ya watoto yatima pamoja na wanaoishi katika mazingira magumu na toa msaada kwa wafanyakazi wa hapo.
- Anzisha kundi la kushona/kufuma ili kutengeneza nguo kwa ajili ya wahitaji.
- Msomee Biblia kwa sauti mtu asiyeona au asiyeweza kusoma.
- Endesha usiku wa vijana nyumbani kwako.
- Toa makazi kwa watu walionyanyaswa.
- Gawa baadhi ya vitabu kwenye makazi ya watoto.

- Panga na kusimamia siku ya kufurahi kwa ajili ya watoto na wenye mahitaji maalum pamoja na familia zao.
- Andaa siku ya kufanya usafi katika jamii.
- Anzisha chama cha afya katika kanisa lako. Alika marafiki na majirani.
- Mwulize mtu kama angependa kuungana na wewe kutazama mkanda wenye ujumbe wa kiroho. Kadiri mnavyotazama pamoja, omba kwamba Roho Mtakatifu anene na moyo wa mtu huyo.
- Buni mradi wako mwenyewe.

Kwa vitendea kazi zaidi juu ya ushuhudiaji, tembelea tovuti ifuatayao: www.revivalandreformation.org/resources/witnessing.

## Ahadi za Biblia za Kudai kwenye Maombi

### *Ahadi za Roho Mtakatifu*

"Mwombeni Bwana mvua wakati wa masika, naam, Bwana afanyaye umeme, naye atawapa manyunyu ya mvua, kila mtu atapewa nyasi kondeni." *Zakaria 10:1*

"Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?" *Luka 11:13*

"Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia… Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu." *Yohana 14:26; 16:8*

"Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba. Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya." *Yohana 14:12–14*

"Akajibu akaniambia, akisema, Hili ndilo neno la Bwana kwa Zerubabeli, kusema, Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi." *Zakaria 4:6*

## Ahadi Kwamba Mungu Hujibu Maombi

"Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa." *Yohana 15:7*

"Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji." *Waebrania 4:16*

"Kwa sababu hiyo nawaambia, Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." *Marko 11:24*

"Ukaniite siku ya mateso; Nitakuokoa, na wewe utanitukuza." *Zaburi 50:15*

"Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lo lote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni." *Mathayo 18:19*

"Na yo yote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea." *Mathayo 21:22*

"Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya." *Yohana 14:13, 14*

"Tena siku ile hamtaniuliza neno lo lote. Amin, amin, nawaambia, Mkimwomba Baba neno lo lote atawapa kwa jina langu. Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu." *Yohana 16:23, 24*

"Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba." *1 Yohana 5:14, 15*

**Ahadi Kuhusu Nguvu ya Mungu**

"Kuna neno gani lililo gumu la kumshinda Bwana? Kwa muhula wake nitakurudia, wakati huu huu mwakani, na Sara atapata mwana wa kiume." *Mwanzo 18:14*

"Bwana atawapigania ninyi, nanyi mtanyamaza kimya." *Kutoka 14:14*

"Yesu akawakazia macho, akasema, Kwa wanadamu haiwezekani, bali kwa Mungu sivyo; maana yote yawezekana kwa Mungu." *Marko 10:27*

"Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya." *1 Wathesalonike 5:24*

"Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote, Na ya kuwa makusudi yako hayawezi kuzuilika." *Ayubu 42:2*

"Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu? Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?" *Warumi 8:31, 32*

"Mungu si mtu, aseme uongo; Wala si mwanadamu, ajute; Iwapo amesema, hatalitenda? Iwapo amenena, hatalifikiliza?" *Hesabu 23:19*

"Je! Wewe hukujua? Hukusikia? Yeye Mungu wa milele, Bwana, Muumba miisho ya dunia, hazimii, wala hachoki; akili zake hazichunguziki. Huwapa nguvu wazimiao, humwongezea nguvu yeye asiyekuwa na uwezo. Hata vijana watazimia na kuchoka, na wanaume vijana wataanguka; bali wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia." *Isaya 40:28–31*

**Ahadi za Uongozi wa Mungu**

"Je! Si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendako." *Yoshua 1:9*

"Na tazama, mimi nipo pamoja nawe, nitakulinda kila uendako, nami nitakuleta tena mpaka nchi hii, kwa maana sitakuacha, hata nitakapokufanyia hayo niliyokuambia." *Mwanzo 28:15*

"Tazama, mimi namtuma malaika aende mbele yako, ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipokutengezea." *Kutoka 23:20*

"Lakini huko, kama mkimtafuta Bwana, Mungu wako, utampata, ukimtafuta kwa moyo wako wote, na roho yako yote." *Torati 4:29*

"Niite, nami nitakuitikia, nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua." *Yeremia 33:3*

"Kila bonde litainuliwa, Na kila mlima na kilima kitashushwa; Palipopotoka patakuwa pamenyoka, Na palipoparuza patasawazishwa; Na utukufu wa Bwana utafunuliwa, Na wote wenye mwili watauona pamoja; Kwa kuwa kinywa cha Bwana kimenena haya." *Isaya 40:4, 5*

"Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea; Nitakushauri, jicho langu likikutazama." *Zaburi 32:8*

"Naye Bwana, yeye ndiye atakayekutangulia, atakuwa pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha; usiogope wala usifadhaike." *Torati 31:8*

"Ni nani amchaye Bwana? Atamfundisha katika njia anayoichagua." *Zaburi 25:12*

"Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atayanyosha mapito yako." *Mithali 3:5, 6*

"Na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri. Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui." *Isaya 58:10, 11*

"Nao watatoka nje na kuitazama mizoga ya watu walioniasi; maana funza wao hatakufa, wala moto wao hautazimika nao watakuwa chukizo machoni pa wote wenye mwili." *Isaya 65:24*

**Ahadi za Moyo Uliobadilishwa**

"Nami nitawapa moyo, wanijue ya kuwa mimi ni Bwana; nao watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao; kwa maana watanirudia kwa moyo wao wote." *Yeremia 24:7*

“Bwana, Mungu wako, atautahiri moyo wako, na moyo wa uzao wako, ili umpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, upate kuwa hai.” *Torati 30:6*

“Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama.” *Ezekieli 36:26*

“Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu.” *Wafilipi 1:6*

“Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya.” *1 Wakorintho 5:17*

“Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.” *Wagalatia 2:20*

“Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya.” *1 Wathesalonike 5:23, 24*

**Ahadi za Msamaha**

“Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao.” *1 Nyakati 7:14*

“Kwa maana Wewe, Bwana, U mwema, Umekuwa tayari kusamehe, Na mwingi wa fadhili, Kwa watu wote wakuitao.” *Zaburi 86:5*

“Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu.” *Marko 11:25*

"Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi." *Waefeso 4:32*

"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." *1 Yohana 1:9*

"Haya, njoni, tusemezane, asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu." *Isaya 1:18*

"Mimi, naam, mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe, wala sitazikumbuka dhambi zako." *Isaya 43:25*

"Maana nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena." *Yeremia 31:34*

"Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake." *Waefeso 1:7*

**Ahadi za Ushindi Dhidi ya Dhambi**

"Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu." *1 Yohana 5:4*

"Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda." *Warumi 8:37*

"Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo." *1 Wakorintho 15:57*

"Usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu." *Isaya 41:10*

"Zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu." *Waefeso 6:16*

"Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu." *Wagalatia 2:20*

"Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema." *Wafilipi 2:13*

"Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili." *Wagalatia 5:16*

"Naye Mungu wa amani atamseta Shetani chini ya miguu yenu upesi. Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na iwe pamoja nanyi. Amina." *Warumi 16:20*

"Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu." *Warumi 12:2*

"Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake." *1 Yohana 2:15*

**Ahadi za Uponyaji**

"Akawaambia, Kwamba utaisikiza kwa bidii sauti ya Bwana, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele zake, na kutega masikio usikie maagizo yake, na kuzishika amri zake, mimi sitatia juu yako maradhi yo yote niliyowatia Wamisri; kwa kuwa Mimi ndimi Bwana nikuponyaye." *Kutoka 15:20*

"Makomeo yako yatakuwa ya chuma na shaba; Na kadiri ya siku zako ndivyo zitakavyokuwa nguvu zako." *Torati 33:25*

"Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana, Wala usizisahau fadhili Zake zote. Akusamehe maovu yako yote, Akuponya magonjwa yako yote, Aukomboa uhai wako na kaburi, Akutia taji ya fadhili na rehema, Aushibisha mema uzee wako, Ujana wako ukarejezwa kama tai." *Zaburi 103:2–5*

"Usiwe mwenye hekima machoni pako; Mche Bwana, ukajiepushe na uovu. Itakuwa afya mwilini pako, Na mafuta mifupani mwako." *Mithali 3:7, 8*

"Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu. Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona." *Isaya 53:3-5*

"Uniponye, Ee Bwana, nami nitaponyeka; uniokoe, nami nitaokoka; kwa maana wewe ndiwe uliye sifa zangu." *Yeremia 17:14*

"Maana nitakurudishia afya, nami nitakuponya jeraha zako, asema Bwana, kwa sababu wamekuita, mwenye kutupwa, wakisema, Ni Sayuni, ambao hapana mtu autakaye." *Yeremia 30:17*

"Tazama, nitauletea afya na kupona, nami nitawaponya; nami nitawafunulia wingi wa amani na kweli." *Yeremia 33:6*

"Lakini kwenu ninyi mnaolicha jina langu, jua la haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa zake; nanyi mtatoka nje, na kucheza-cheza kama ndama wa mazizini." *Malaki 4:2*

"Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa." *Yakobo 5:14, 15*

**Ahadi kwa ajili ya Nguvu za Kufanya Mapenzi ya Mungu**

"Kwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku. Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana.

Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele." *2 Wakorintho 4:16-18*

"Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho." *Wagalatia 6:9*

"Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu." *Wafilipi 4:13*

"Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema." *Wafilipi 2:13*

"Naye akaniambia, Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu." *2 Wakorintho 12:9*

**Ahadi Kuhusu Kuwa Mashahidi wa Mungu**

"Msiogope wala msifanye hofu; je! Sikukuhubiri haya zamani na kuyaonyesha? Na ninyi ni mashahidi wangu. Je! Yuko Mungu zaidi yangu mimi? Hakika hapana Mwamba; mimi sijui mwingine." *Isaya 44:8*

"Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, Na utukufu wa Bwana umekuzukia." *Isaya 60:1*

"Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho." *2 Wakorintho 5:18*

"Lakini Bwana akaniambia, Usiseme, Mimi ni mtoto; maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema kila neno nitakalokuamuru." *Yeremia 1:7*

"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi." *Matendo 1:8*

“Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu.” *1 Petro 2:9*

“Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu.” *1 Petro 3:15*

**Sherehe ya Siku ya Sabato**

- Andaa Sabato ya mwisho ya Siku Kumi za Maombi ili kusherehekea wema wa Mungu na uweza mkuu. Eleza jinsi ulivyopata uzoefu wa nguvu ya maombi na ushiriki uelewa muhimu wa kiroho uliopatikana katika siku kumi zilizopita. Furahia yale ambayo Mungu amefanya, anayofanya na atakayofanya.

- Mahitaji ya kila kanisa ni ya pekee, kwa hivyo tafadhali fanya kazi na viongozi mahalia ili kutengeneza mpango mahususi kwa ajili ya kanisa lako. Hapa kuna baadhi ya vitu vinavyowezekana kujumuisha katika ibada yako ya Sabato ya mwisho.

**Mada ya Mwaka 2025:**

Bali Wewe Usalipo ... (Kanuni za Maombi Kutoka kwa Yesu)

**Mafungu ya Mada:**

"Bwana, tufundishe sisi kusali."

Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.

**Pendekezo la Nyimbo:**

- Mtazame Mwokozi (Vd. 212 & Vk. 137)
- Kungoja Ahadi (Vk. 306)
- Ni Salama Rohoni Mwangu (Vd. 127 & Vk. 327)
- Uishi Ndani Yangu (Vd. 147 & Vk. 339)
- Yu Hai, Yu Hai (Vd. 167 & Vk. 93)

**Mapendekezo ya Hubiri:**

Hubiri Moja: Hebu mchungaji, mzee au kiongozi wa maombi ahubiri hubiri kuhusu jinsi tutakavyoweza kuiishi kanuni za Sala ya Bwana.

**[AU]**

Muhtasari Mfupi: Hebu wale walioshiriki katika Siku Kumi za Maombi wapokezane kutoa muhtasari mfupi (dakika 1-2) kwa kila mwongozo wa siku 10 za maombi ya kila siku. Wasilisha kichwa, fungu kuu na wazo kuu. (Jiandaeni mapema ili muhtasari ubakie ndani ya dakika 1-2. Kwa watu wengi, dakika moja ni maneno 125–150 yanayozungumzwa.)

**[AU]**

Mazungumzo Mafupi Juu ya Mada Fanani: Orodhesha washiriki watatu wa vikundi vya rika tofauti ili kutoa mawasilisho mafupi (dakika 5-10) kuhusu mada iliyochaguliwa, kama vile Sala ya Bwana au kisa cha maombi kutoka ndani ya Biblia.

**Mawazo Mengine ya Programu:**

Shuhuda za washiriki juu ya maombi yaliyojibiwa, Muda wa maombi ya vikundi vidogo, Matangazo ya maombi na shughuli zijazo za huduma, Kisa cha watoto kuhusu maombi, Chaguzi za nyimbo maalum, n.k.

## Mahitaji ya Kuombewa kwa kanisa la ulimwengu

- Bwana, tunaomba uruhusu ule uamsho wa ucha Mungu wa zamani ulikumbe kanisa Lako katika siku hizi za mwisho. Tuwezeshe kusimama hata kama mbingu zianguke. Ruhusu uamsho huu uanze na mimi.
- Bwana tunaomba utuweze kuwa thabiti katika maombi kila siku, kwa mtu binafsi na kwa familia.
- Bwana, tunaomba utufungue macho yetu ili kuona uharibifu maishani mwetu. Mambo ambayo yanatuzuia tusiweze kukaza macho yetu Kwako. Tupatie mioyo ya kupenda kukuabudu Wewe tu.
- Bwana, tunaomba utusaidie tukuruhusu Wewe kutuamsha kila siku asubuhi, bila kujali ni mapema kiasi gani, ili kwamba tuweze kuwa na muda mzuri pasipo haraka katika Neno Lako na maombi.
- Tunaomba kwamba utuwezeshe kukujia jinsi tulivyo, kwa hisia zetu zote, mapungufu yetu, dhambi zetu, mahitaji yetu na tukuruhusu Utupende, utubadilishe na kutuumba upya ukitufanya kuwa vile Upendavyo tuwe.
- Bwana, tufundishe namna ya kuomba kila siku kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu.
- Tunaomba kwa ajili ya mvua ya masika ya Roho Mtakatifu ili kuimarisha ushuhudiaji wetu na kutuwezesha ili kujihusisha katika kazi ambayo Umetupatia kabla ya ujio Wako.
- Tufundishe jinsi ya kuzipenda familia zetu kwa kujitoa kafara na namna ya kuwafanya wanafunzi kwa ajili ya Ufalme, kuanzia kwa watoto wetu na wapendwa wetu.
- Tunaomba utupatie hekima ya kulichunguza, kulielewa na kulitii Neno la Mungu. Tunaomba utufundishe kuyapambanua vyema maneno ya ukweli na kwa uaminifu kuwashirikisha wengine Neno Lako.
- Bwana, tunaomba uamshe upya hali yetu ya kuyathamini maagizo yanayopatikana katika maandiko yaliyovuviwa ya Ellen G. White.

- Tunaomba kwa ajili ya uhuru wa dini na haki ya dhamiri ulimwenguni kote. Bwana, tunaomba ufungue milango kwa ajili ya utangazwaji wa Neno Lako katika maeneo yaliyofungwa.
- Bwana, tunaomba kanisa Lako ulimwenguni liitikie wito wa kutangaza ujumbe wa malaika watatu kwa kila taifa, lugha na jamaa. Tuoneshe jinsi ya kukaza mafundisho haya yote katika upendo na haki ya Kristo Yesu.
- Bwana, tunaomba uwawezeshe Waadventista wa Sabato wote ulimwenguni kuitika "Nitakwenda" na kuuchukua mwito ili kukutumikia na kuhubiri habari njema ya wokovu.
- Tunaomba kwamba Waadventista wa Sabato wote ulimwenguni wawe tayari kusaidia na kutia moyo wale wote wanaopita katika adha ya maumivu maishani. Tunaomba utupatie ujasiri, ubunifu na roho isiyo na ubinafsi pale jirani zetu wanapokuwa wakituhitaji sana.
- Tunawaombea wale wote walioathirika kifedha kwa sababu ya mabadiliko ya kiuchumi.
- Bwana, tunaomba uwaoneshe waumini makanisani namna ya kuwaidia wale ambao wanapambana na matatizo ya afya ya akili au ya kutengwa.
- Tunawaombea wachungaji pamoja na makanisa kupata namna ya kuwezesha waumini kuomba pamoja kwa bidii. Bwana, tunaomba uliunganishe kanisa Lako pamoja katika ibada na huduma.
- Tunaomba kwa ajili ya uamsho wa kiroho miongoni mwa vijana wa kanisa la Waadventista wa Sabato wanaohudhuria katika vyuo vikuu na taasisi nyingine za elimu ulimwenguni kote. Tunakuomba Bwana, uwafanye kuwa mabalozi wakereketwa kwa ajili ya Yesu.
- Tunaombea asilimia 69 ya watu ulimwenguni ambao hawajapokea mafundisho ya Yesu yasiyochafuliwa.

- Tunaombea watu milioni 62 katika miji 28 ambayo haijafikiwa au imefikiwa kwa uchache katika nchi ya Urusi (Divisheni ya Euro-Asia.)

- Tunaomba Mungu ainue wamisionari jasiri walio tayari kufanya kazi kati ya makundi 746 yaliyopo katika nchi 20 za Mashariki ya kati.

- Bwana, tafadhali uinue wanafunzi Wa-Aldensia ambao wako tayari kukutumikia katika maeneo magumu.

- Tunawaombea waumini wa kanisa la Waadventista wa Sabato wanaokabiliwa na mateso na kutupwa gerezani kwa sababu ya Imani yao.

- Tunaomba kwa ajili ya watu milioni 202 waliopo katika miji 41 iliyofikiwa kwa uchache katika Divisheni ya Kusini mwa Asia-Pasifiki wapate kumfahamu Yesu.

- Tunaomba kwa ajili ya Idara ya Shule ya Sabato na Huduma Binafsi ya kila kanisa mahalia kadiri wanavyotafuta mpango wa Mungu na kuwafikia walio nje katika jamii kwa huduma za upendo, mafunzo ya Biblia, na ushuhuda binafsi.

- Tunaomba kwa ajili ya shirika la misaada la Waadventista wa Sabato (ADRA) kadiri wanavyokabiliana na mahitaji ya watu ulimwenguni kote.

- Tunawaombea watu milioni 16 katika miji 6 ambayo imefikiwa kwa uchache sana katika Divisheni ya Kusini mwa Pasifiki.

- Tunaomba kuwa Roho Mtakatifu atusaidie kufahamu jinsi ya kufikia watu milioni 406 katika miji 105 ya Divisheni ya Kaskazini mwa Asia-Pasifiki ambayo haijafikiwa au imefikiwa kwa uchache sana.

- Bwana, tunaomba ubariki Huduma ya Uchaplensia ya kanisa la Waadventista wa Sabato iweze kuhamasisha wahudumu pamoja na waumini wenye shauku ya kuhudumia watu waliopo magerezani.

- Ee Bwana, tunaombea waalimu wa Shule ya Sabato. Wasaidie kufahamu umuhimu wa kazi yao kwa watoto wetu.
- Bwana, tunaomba uongozi Wako kwa ajili ya vituo vingi vya mvuto, programu za afya na familia, pamoja na chama cha Watafutanjia ulimwenguni kote.
- Bwana, tunaomba utuoneshe jinsi ya kupeleka machapisho yaliyojawa na ukweli kwa jamii zetu. Tunaomba kwamba uwajalie kuyasoma na kwamba Roho Mtakatifu alete ushawishi katika ukweli wa Biblia.

- Bwana, tunaomba ulinzi Wako kwa wamisionari wanaofanya kazi katika maeneo hatarishi.
- Tunakuomba uinue wainjilisti wa vitabu, wanafunzi wa kujitolea, waandishi, wataalam wa mitandao ya kijamii, pamoja na wafadhili watakaosaidia kueneza maneno ya matumaini na uzima.
- Tunaomba kwa ajili ya shule za kanisa la Waadventista wa Sabato, wanafunzi, pamoja na waalimu ulimwenguni kote. Hebu shule hizi zifundishe kwa uaminifu kweli za Biblia na kuwaongoza vijana katika utume, huduma na kushiriki uhusiano na Kristo.
- Bwana, tupatie hekima ya kufikia tamaduni zingine ambazo hazina shauku ya dini. Hebu Roho wako Mtakatifu aangushe kuta ambazo zinazunguka roho hizo.
- Tunakuomba utubariki kadiri tunavyowaendea watu waliofungwa katika ibada ya mizimu, ibada ya sanamu na imani katika vitu vinavyoonekana. Tusaidie kuelewa mtazamo wao wa kidunia na kisha kuwatambulisha kwa Mwokozi wao binafsi.
- Bwana, tunakuomba ulete uvuvio kwa kanisa la Waadventista wa

Sabato ulimwenguni kote wapate kuomba kwa namna ambayo hawajawahi kuomba. Tufundishe kudai ahadi Zako na kutazamia kwamba utahamisha milima zaidi tunapoomba.

- Tunaomba kwa ajili ya makundi 514 ya watu katika nchi 18 za Divisheni ya Bahari ya Hindi Kusini mwa Afrika. Tafadhali waongoze katika ukweli wa Biblia.
- Tunakuomba utuoneshe jinsi ya kuyafikia mahitaji ya kiroho ya wakimbizi. Hebu kanisa letu lifahamike kwa upendo wetu kwa watu wote, bila kujali kuwa ni akina nani au wanatoka wapi.
- Tunakuomba uwainue wamisionari wa mijini wapate kuanzisha makanisa kwa makundi 806 ya watu katika nchi 20 za Divisheni ya Ulaya (Inter—Europe Division.)
- Tunakuomba uinue jeshi la watendakazi watakaoanzisha makanisa kati ya makundi 948 ya watu katika nchi 38 za Divisheni ya Amerika (Inter-America Division)
- Bwana, tunakuomba uandae vijana watakaojihusisha katika kuanzisha makanisa kati ya makundi 789 ya watu katika nchi 9 za Divisheni ya Kaskazini mwa Amerika.
- Tunakuomba uandae watu wa kujitolea ili kuhudumia makundi 70 ya watu katika Fildi ya Israeli.
- Tunakuomba uinue matabibu wa kimisionari ili kuanzisha makanisa kati ya makundi 830 ya watu katika nchi 11 za Divisheni ya Mashariki-Kati mwa Afrika.
- Tunakuomba uinue mashujaa wa maombi wapate kuombea makundi 2,568 ya watu katika nchi 4 za Divisheni ya Kusini mwa Asia.
- Tafadhali wezesha familia zetu kudhihirisha upendo Wako

majumbani mwetu na katika jamii zinazotuzunguka. Tunaomba ulete maelewano majumbani, ponya mahusiano yaliyovunjika, linda wahanga wa unyanyasaji na dhihirisha uweza Wako utakasao katika hali zinazoonekana kutokuwa na matumaini.

- Tunakuomba uinue wauguzi na madaktari wa kuanzisha makanisa mapya kati ya makundi 1,978 ya watu katika nchi 22 za Divisheni ya Magharibi-Kati mwa Afrika.

- Tunaomba kwa ajili ya watu milioni 49 katika miji 19 ambayo hijafikiwa au imefikiwa kwa uchache sana katika Divisheni ya Trans-Europe.

- Tunaomba kwa ajili ya Watoto wetu. Tafadhali wawezeshe kusimama kwa ujasiri kukutetea wanapokabiliana na vikwazo na misukumo. Wasaidie kufanya chaguzi sahihi na kusimamia ukweli.

- Tunaomba utufundishe kufuata mfano wa Yesu usiokuwa na ubinafsi kwa kufikia mahitaji ya kila siku ya watu wanaotuzunguka. Tuwezeshe kuhudumu kama wamisionari matabibu, watu wanaojitolea katika jamii na rafiki za watu wenye uhitaji.

**Bali Wewe Usalipo …**

Siku ya 01

# Kaeni Ndani Yangu

**Fungu Elekezi:** *"Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote"* (Yohana 15:5).

**Kudumu Kuunganishwa—Hitaji kwa Ajili ya Kuzaa Matunda**

Baada ya kuhitimu niliitwa kutumika kwenye mtaa wenye makanisa madogo matatu. Ulikuwa ni wakati wa majira ya baridi. Moja ya makanisa lilikuwa na washiriki wazee. Katika kila Sabato hasa yenye tukio maalum, tulikuwa na watu takribani 40. Kwenye Sabato ya kawaida tulikuwa na watu takribani 10.

Sabato moja kulikuwa na baridi sana, ilikuwa takribani nyuzi joto -30 na watu tisa walihudhuria: familia yangu ya watu wanne na wengine watano. Niliwaza, je, nihubiri? Mzee kiongozi wa kanisa, mwanamke ambaye alikuwa na umri wa takribani miaka 90, alisema, "Tunarudisha zaka, kwa hiyo inakulazimu kuhubiri." Kwa hiyo nilihubiri.

Hubiri langu lilitoka katika kitabu cha Yohana 15:4–8. Katika aya nne Yesu anarudia "Kaeni ndani Yangu" mara tatu. Katika utamaduni wa Kiebrania, jambo linaporudiwa mara tatu ni muhimu sana yaani muhimu mno. Nilisisitiza kwamba cha muhimu sana si kile tunachokifanya katika maisha ya Kikristo. Tunapoitwa kutumika, hatuwezi kuwa na matokeo kwa uwezo wetu wenyewe. Hata hivyo Yesu alitoa Neno Lake kwamba ikiwa tutadumu kukaa ndani Yake, chochote tutakachoomba, tutatendewa. Hakuna utata; ni uthibitisho wa mafanikio kwa asilimia 100.

"Kwa hiyo," niliwaambia wasikilizaji, "si kile tunachofanya kiletacho mabadiliko, bali kile ambacho Mungu anaweza kufanya."

Mwandishi Ellen G. White anaeleza, "Si uwezo ulio nao sasa, au utakaowahi kuwa nao, utakaokupa  mafanikio. Ni yale ambayo Bwana anaweza kufanya kwa ajili yako. Tunahitaji kuwa na imani kidogo mno katika kile ambacho mwanadamu anaweza kufanya, bali kuwa na imani zaidi katika kile ambacho Mungu anaweza kufanya kwa kila nafsi inayoamini" (*Christian Service*, uk. 262).

Niliwaambia kusanyiko langu dogo kwamba maombi "ni siri ya kuwa na nguvu za kiroho" (*Prayer,* uk. 12). Yanatuunganisha na (Chanzo cha nguvu" (*Steps to Christ*, uk. 95). Ni silaha yenye ufanisi zaidi dhidi ya mashambulizi ya Shetani (*Testimonies for the Church*, vol. 1 uk. 295, 296, 345, 346).

Niliwaambia juu ya ahadi ambayo Yesu aliitoa katika Mathayo 18:19, 20. "Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lo lote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni. Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao." Haisemi "ikiwa 200 au 300 wataomba" bali "ikiwa 2 au 3 wataomba" kwa ajili ya jambo fulani kwa mapatano, katika umoja. Na sio "Ninaweza nikalifanya" bali kwa uwazi kabisa "*Nitalifanya*."

Niliwaambia wasikilizaji wangu wachache, "hatuwezi kuchagua kutofanya kitu. Lazima tuombe na kufanya kazi, kisha Mungu ataleta matokeo kama alivyoahidi." Lilikuwa hubiri bora juu ya nguvu ya maombi.

Tulipokuwa tukirudi nyumbani, nilimwambia mke wangu, "Tunahitaji kuhama. Hakuna tumaini la ukuaji au kwa kweli wa kitu chochote katika kanisa hili." Alinikumbusha hubiri langu, kwa ahadi ya Yesu, na kisha akaniuliza, kwa nini usiwaite katika maombi?" Nilisita kufanya hivyo. Wale wanawake wachache walikuja kila asubuhi saa 12:30 asubuhi. Ili kuomba pamoja kwa ajili ya Roho Mtakatifu, ukuaji wa kanisa, familia, jiji, mpango wa Mungu kwa kanisa letu na uwazi kwa kile tunachotaka

kukifanya. Miezi mitatu baadaye kanisa lilikuwa na watu waliohudhuria takribani 120.

Mungu anakuita ili udumu ndani Yake, omba bila kukoma, baki ukiwa umeunganishwa na kutembea Naye. Anakualika ukae ndani Yake, na lazima kila siku umkaribishe akae ndani yako. Hicho ndicho chanzo chako pekee cha nguvu ya kweli. Huo ndiyo usalama wako. Maadamu umeunganishwa na Mungu, Shetani hana nguvu juu yako. Kristo ndani yako na wewe ndani Yake ni njia moja ya kukua na kufanikiwa.

Tuombe pamoja.

**Muda wa Maombi (Dakika 30–45)**

*Vikundi vyote vya maombi vina njia tofauti za kuomba pamoja. Tunawahimiza kutumia dakika 30-45 zinazofuata katika maombi ya pamoja, kwa njia yoyote ambayo Roho Mtakatifu anaongoza. Tunahimiza maombi mafupi ya wazi (sentensi 1-3). Hii inaruhusu watu wengi zaidi kuomba mara nyingi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya kuomba kupitia Maandiko kulingana na mada. Unaweza kuomba kupitia aya zingine pia na kujumuisha masomo mengine katika wakati wako wa maombi. Tazama Mwongozo wa Kiongozi na Maombi ya Maombi ya Kanisa Ulimwenguni kwa mawazo ya maombi.*

**Kuomba Sawasawa na Neno la Mungu—Yohana 15:5**

"Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote."

**"Kaeni Ndani Yangu Nami Ndani Yenu"**

*Bwana Yesu, tunaomba utufundishe namna ya kukaa ndani Yako kila siku. Pasipo Wewe, sisi ni kama matawi yaliyokufa kwa kutenganishwa kutoka kwenye mzabibu utoao uzima. Tembea pamoja nasi, fanya kazi*

*ndani yetu, zungumza kupitia sisi. Tunaomba uishi ndani ya mioyo yetu na Uupende ulimwengu kupitia kwetu.*

**“Mtazaa Matunda Mengi”**

*Bwana, tunajua kwamba haki yote yatoka Kwako. Otesha tunda la Roho katika maisha yetu. Tujaze na upendo Wako, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu upole na kiasi. Ruhusu maisha yetu yaakisi tabia Yako isiyo na waa kwa kila mtu tunayekutana naye.*

**“Pasipo Mimi Hamwezi Kufanya Neno Lolote”**

*Bwana, tunajua kwamba matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi. Tunavunja ahadi zetu, tunawaudhi adui zetu, na kuwasaliti wale tunaowapenda. Pasipo Wewe, sisi tu wanyonge na waliopotea. Tunahitaji upendo Wako, uvumilivu Wako na neema Yako mioyoni mwetu kila siku. Tutunze karibu katika upande Wako.*

**Mapendekezo ya Maombi Zaidi**

**Shukrani na Sifa:** Shukuruni kwa baraka mahususi na Msifuni Mungu kwa wema Wake.

**Kuungama:** Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

**Uongozi:** Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

**Kanisa Letu:** Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

**Mahitaji ya Eneo Mahalia:** Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

**Sikiliza na Uitike:** Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

**Mapendekezo ya Nyimbo**

*Nyimbo za Kristo*:

- Kaa Nami (19 Vk & 91 Vd)
- Ni Wako Bwana (159 Vk & 144 Vd)
- Moyoni (400 Vk & 211 Vd)

Siku ya 02

# Utufundishe Kuomba

“Ikawa alipokuwa mahali fulani akiomba, alipokwisha, mmoja katika wanafunzi wake alimwambia, Bwana, ‘tufundishe sisi kusali’” (Luka 11:1).

**Moyo wa Uhai wa Mkristo**

Maombi ni muhimu, tena ni uhai.

“Kila asubuhi tumia muda ili kuanza kazi yako kwa maombi. Usifikiri kuwa muda huu ulipotea, ni muda utakaodumu hata milele. Kwa njia hii mafanikio na ushindi wa kiroho utapatikana” (*Testimonies for the Church*, vol. 7, uk. 194).

Mara nyingi wanafunzi walimshuhudia Yesu akiomba. Waligundua kuwa alikuwa na maisha ya maombi tofauti na ya kwao. Wanafunzi hawa walikuwa watu wema wa kiroho. Walikuwa wameisalimisha mioyo yao na walitaka kumtumikia Mungu. Walienda kanisani, waliitunza Sabato, walirudisha zaka kwa uaminifu na walikula chakula kisicho najisi. Kila mtu huko Israeli, hususani wanafunzi, alijua kuomba, sawa?

Tunadhani tunajua kuomba. Hata watoto wanajua kuomba. Lakini wanafunzi walipomtazama Yesu akiomba—na walipolinganisha maombi yao na ya Kwake—waligundua kuwa hawakujua jinsi ya kuomba. Hiyo ndiyo sababu iliyowafanya kusema, “Tufundishe kuomba” (Luka 11:1).

Tunafikiri kwamba kuomba ni jambo rahisi mno. Na ni kweli, Mungu atasikiliza ombi rahisi kabisa. Lakini lazima tuendelee kuimarisha maisha yetu ya maombi.

Wanafunzi waligundua kwamba walihubiri, lakini hakuna mtu aliyeguswa. Walijaribu kuponya au kutoa mapepo, lakini hawakuwa na

nguvu. Walimwuliza Yesu, “Je! Wewe unafanyaje?” Yesu alisema, “Kwa kufunga na kuomba.”

Kimsingi Yesu anasema huwezi kufanya mambo kwa hekima yako mwenyewe; ni kwa nguvu ya Mungu tu. Ili uweze kufanikiwa, unapaswa kuomba kwa bidii. Katika kitabu cha Warumi, Paulo anasema kwamba lazima Roho Mtakatifu aombe kwa ajili yetu kwa sababu hatujui hata jinsi ya kuomba (Rum. 8:26).

Maombi ni pumzi ya nafsi. Ni siri ya nguvu za kiroho…. Puuza kufanya maombi, au jihusishe katika maombi kwa kushtukizwa, hapa na pale, kama ionekanavyo kuwa sawa, hapo utapoteza muunganiko wako na Mungu” (*Prayer*, uk. 12, 13).

Yesu alikuwa na maisha ya maombi yenye nguvu na mara nyingi alitumia usiku kucha katika maombi. “Yesu Mwenyewe, alipoishi miongoni mwa wanadamu, mara nyingi alikuwa katika maombi…. Yeye ni kielelezo chetu katika mambo yote…. Ubinadamu Wake uliyafanya maombi kuwa ni hitaji na fursa. Alipata furaha na faraja katika kujumuika na Baba Yake. Na ikiwa Mwokozi wa wanadamu, Mwana wa Mungu, alihisi hitaji la kuomba, ni jinsi gani basi wanadamu wanyonge, watendao dhambi wanapaswa kuhisi umuhimu wa maombi ya bidii na ya kudumu” (*Steps to Christ,* uk. 93, 94).

Yesu alifanya maombi kuwa kipaumbele Chake, kitu cha kwanza kabla siku haijaanza. “Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko” (Marko 1:35). Yesu alikuwa na muda na mahali kwa ajili ya maombi.

Wanafunzi waliposema, “Tufundishe kuomba,” Yesu hakuwaambia, “Ombeni kwa kusema hivi,” kama mantra (maneno ya kurudiarudia). Kwa kweli, aliwaambia waziwazi kwama wasirudierudie maneno yaleyale kila mara walipoomba (Mt. 6:7). Yesu Mwenyewe aliomba ombi tofauti katika Yohana 17, kulingana na hitaji la hali halisi.

"Maombi ni ufunguaji wa moyo kwa Mungu kama kwa rafiki" (*Steps to Christ,* uk. 93). Katika maombi tunafungua mioyo yetu kwa Mungu katika mazungumzo ya kweli, kama majadiliano. Ikiwa unarudia maneno yayo hayo kila mara unapoomba, itakuwa desturi na wala hautakuwa unafikiria kile unachokisema.

Maombi na usomaji wa Neno lazima viende pamoja daima. Kwa njia ya maombi tunaongea na Mungu; kwa njia ya Neno Mungu anaongea na sisi.

Yesu aliishi maisha ya maombi. Aliomba alfajiri na mapema, Alienda mahali maalum kwa ajili ya maombi, na alizungumza kwa uwazi na Mungu. Yeye ni kielelezo chetu. Anatuita ili tuombe kama Yeye.

Hebu na Tuombe Pamoja.

**Muda wa Maombi (Dakika 30–45)**

*Vikundi vyote vya maombi vina njia tofauti za kuomba pamoja. Tunawahimiza kutumia dakika 30-45 zinazofuata katika maombi ya pamoja, kwa njia yoyote ambayo Roho Mtakatifu anaongoza. Tunahimiza maombi mafupi ya wazi (sentensi 1-3). Hii inaruhusu watu wengi zaidi kuomba mara nyingi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya kuomba kupitia Maandiko kulingana na mada. Unaweza kuomba kupitia aya zingine pia na kujumuisha masomo mengine katika wakati wako wa maombi. Tazama Mwongozo wa Kiongozi na Maombi ya Maombi ya Kanisa Ulimwenguni kwa mawazo ya maombi.*

**Kuomba Sawasawa na Neno la Mungu—Luka 11:1**

"Ikawa alipokuwa mahali fulani akiomba, alipokwisha, mmoja katika wanafunzi wake alimwambia, Bwana, 'tufundishe sisi kusali'"

**"Yesu Alikuwa Akiomba Mahali Fulani"**

*Baba, tunaomba utufundishe kuomba kama vile Yesu. Tunakiri kuwa na visingizio na kukengeushwa na kuwa na shughuli nyingi. Tusaidie kuchagua wakati na mahali pazuri pa kukutana Nawe kila siku. Badilisha vipaumbele vyetu na uunde tabia mpya zinazotuongoza katika uwepo Wako.*

**"Bwana, Tufundishe Kuomba"**

*Ndiyo Bwana, tuoneshe namna ya kuomba kama ulivyowaonesha wanafunzi. Asante kwa mfano mzuri wa Sala ya Bwana. Tuoneshe jinsi ya kufanyiza maombi yetu na maisha yetu kwa mfano Wako. Tunaomba utujaze na Roho Mtakatifu, na usikie maombi yetu ili ubadilishe nyumba zetu, kanisa letu, jamii yetu na ufalme Wako.*

**Mapendekezo ya Maombi Zaidi**

**Shukrani na Sifa:** Shukuruni kwa baraka mahususi na Msifunikumsifu Mungu kwa wema Wake.

**Kuungama:** Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

**Uongozi:** Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

**Kanisa Letu:** Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

**Mahitaji ya Eneo Mahalia:** Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

**Sikiliza na Uitike:** Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

**Mapendekezo ya Nyimbo**

- Saa Heri ya Maombi (Vk. 278 & Vd. 135)
- Bwana Sikia (Vk. 402)
- Yesu Kwetu ni Rafiki (Vk. 182 & Vd. 130)

## Siku ya 03

# Kuwa Dhahiri

**Fungu Elekezi:** *"Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi. Basi msifanane na hao; maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi hamjamwomba"* (Mt. 6:7, 8).

**Omba kwa Dhati**

Mwanetu, Ovidiu, alinunua nyumba kwa bei ya chini sana, lakini nyumba hiyo ilikuwa duni na ndogo sana. Ilimlazimu kuirekebishe na kuipanua ili kutosheleza mahitaji ya familia yake. Lakini, bei zilipanda sana. Alisema mara kwa mara hata kukawa na uwezekano mkubwa kutoweza kukamilisha kazi hiyo kutokana na ukosefu wa fedha.

Nilimtaka Ovidiu kuwasilisha mahitaji yao mbele za Mungu kwa sababu Anawajali. Alijibu kwamba ameomba kwa ajili ya nyumba kwa ujumla.

Kisha nikamtaka kuwa dhahiri katika maombi, kuwasilisha hitaji moja baada ya jingine, si kuomba leo kwa kile tutakachokihitaji mwezi ujao au kesho, bali kuomba leo kwa hitaji la leo. Mungu anajibu maombi dhahiri. Mungu hajibu maombi ya jumla.

Usiende kwa Mungu na kusema, "Bwana, okoa jirani zangu." Badala yake, unaweza kusema, "Baba yangu, namwombea jirani yangu Yohana. Tafadhali gusa moyo wake. Pia, tafadhali nipe hekima na fursa za kujenga urafiki naye na kumfikishia habari njema ya injili."

Marko 10:47 humwasilisha Batimayo akimwomba Yesu amsaidie. Anaomba, "Yesu Mwana wa Daudi, unirehemu!" Hilo ni ombi la jumla. Katika aya ya 51 Yesu anamtaka kuwa dhahiri: "Wataka nikufanyie nini?" Batimayo akamwambia, Mwalimu wangu, nataka nipate kuona."

Turudi kwenye kisa changu—kijana wetu akaanza kuomba kwa jambo maalum. Alimwomba Mungu amsaidie kupata timu itakayochimba shimo la msingi wa nyumba hiyo. Kisha akaanza kutafuta. Hata hivyo, timu zote alizowasiliana nazo ziliratibiwa miezi kadhaa kabla na zote zilitoza kati ya dola 18,000 na dola 22,000 za kimarekani. Hatimaye alifanikiwa kufanya mazungumzo na timu moja ili kushusha bei hadi kufikia dola 16,000 na kuja juma lililofuata kuchimba msingi.

Kiongozi wa timu hiyo alikuja, lakini mashine kubwa haikuonekana. Baada ya kungoja asubuhi yote, kiongozi huyo alipoteza subira, akasema hangeweza kurudi kwa miezi mitatu na akaondoka. Mwanetu alihuzunika sana. Hakuwa na suluhisho lolote.

Hatimaye, Ovidiu alimwomba Mungu hasa kwa ajili ya timu ya kuchimba shimo haraka na kwa bei nzuri. Alipomaliza sala yake, jirani yake wa karibu alimkaribia.

Jirani: “Habari ya leo.”

Ovidiu: “Salama. Nipo tu natafuta timu ya kuchimba shimo kwa ajili ya msingi wangu.”

Jirani: “Naam, nina timu inayochimba shimo la nyumba yangu hivi sasa. Waulize. Labda wanaweza kufanya na kwako pia.”

Kwa haraka Ovidiu alikimbilia kwa jirani na kuuliza.

Kiongozi wa timu alijibu: “Naam, kwa kuwa tayari tuko hapa na vifaa vyetu vizito, punde tu tunapomaliza hapa, tunaweza kuja kufanya kazi yako.”

Ovidiu: Je! Unaweza kuja kunipa makadirio?

Baada ya kuangalia, kiongozi wa timu hiyo alisema, “Nitaifanya kwa dola za kimarekani 2,500.”

Furaha iliyoje! Ovidiu aliona kwamba Mungu alikuwa amekwisha kuandaa jibu na alikuwa akimsubiria Ovidiu kuomba kwa ajili yake.

"Maombi ni kuufungua moyo kwa Mungu kama kwa rafiki" (*Steps to Christ*, uk. 93). Mungu anakuita ili kuwa na mazungumzo ya wazi pamoja Naye, kuwasilisha mahitaji yako kwa njia iliyo wazi na dhahiri kabisa. Anataka uwe na imani Kwake, utarajie majibu kulingana na upendo Wake, hekima na ahadi Yake. Atajibu kwa wakati na kwa njia Yake, lakini ikiwa utamngoja kwa imani, utajua kwamba jibu Lake ni jibu lililo bora zaidi.

Hebu na Tuombe Pamoja

*Vikundi vyote vya maombi vina njia tofauti za kuomba pamoja. Tunawahimiza kutumia dakika 30-45 zinazofuata katika maombi ya pamoja, kwa njia yoyote ambayo Roho Mtakatifu anaongoza. Tunahimiza maombi mafupi ya wazi (sentensi 1-3). Hii inaruhusu watu wengi zaidi kuomba mara nyingi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya kuomba kupitia Maandiko kulingana na mada. Unaweza kuomba kupitia vifungu vingine pia na kujumuisha masomo mengine katika wakati wako wa maombi. Tazama Mwongozo wa Kiongozi na Maombi ya Maombi ya Kanisa Ulimwenguni kwa mawazo ya maombi.*

**Kuomba Sawasawa na Neno la Mungu—Mathayo 6:7, 8.**

"Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi. Basi msifanane na hao; maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi hamjamwomba."

**"Msipayuke-payuke"**

*Mungu wetu, tunaomba utufundishe kuongea na Wewe kama vile kwa rafiki. Wakati mwingine maombi yetu huanguka katika mwelekeo wa kuchosha na inaonekana kwamba maneno yetu hayaendi juu zaidi*

*kuvuka dari. Tunaomba utuamshe kiroho! Tusaidie kuhisi ukweli wa uwepo Wako karibu nasi.*

**“Baba Yenu Anajua Mnayohitaji”**

*Bwana Mpendwa, tayari unajua kila kitu kutuhusu. Unajua hofu zetu, matumaini yetu, nguvu zetu na udhaifu wetu. Mara nyingi tunaomba kwa ajili ya matamanio rahisi kama vile chakula au fedha au mafanikio, lakini Unajua mahitaji yetu ya kina zaidi. Asante kwa kuwa Roho hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa na maneno yetu. Tunakuamini kujibu kwa njia ambazo hatuwezi kufikiria!*

**Mapendekezo ya Maombi Zaidi**

**Shukrani na Sifa:** Shukuruni kwa baraka mahususi na Msifuni Mungu kwa wema Wake.

**Kuungama:** Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

**Uongozi:** Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

**Kanisa Letu:** Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

**Mahitaji ya Eneo Mahalia:** Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

**Sikiliza na Uitike:** Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

**Mapendekezo ya Nyimbo**

- Kungoja Ahadi (Vk. 306)
- Ninamjua Nimwaminiye (Vk. 303)

Siku ya 04

# Maombi Yasiyojibiwa (Na Imani)

**Fungu Elekezi:** *"Bali wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya"* Isa. 40:31a).

**Kungojea …**

Kusubiri si kitu cha kufurahisha. Nani anapenda kusubiri? Kusubiri katika ofisi ya daktari, kusubiri mstarini, kusubiri ndege iliyochelewa kwenye uwanja wa ndege, kusubiri mtu ambaye amechelewa kwenye mkutano.

Ibrahimu alilazimika kusubiri kwa miaka 25 ili kupata majibu ya ombi lake. Musa alingoja miaka 40 ili Mungu aingilie kati hatimaye. Yusufu alikuwa mtumwa kwa miaka kadhaa kisha akakaa gerezani miaka michache—si mahali pa kufurahisha pa kungojea kuingilia kati kwa Mungu! Kuna mifano mingi ya kusubiri msaada katika Biblia.

Japokuwa kungojea huleta changamoto kwenye subira yetu, Biblia inasema kwamba sifa moja ya watu wa Mungu ni subira. Vivyo hivyo katika maombi. Mara nyingi, tunalazimika kusubiria majibu.

"Kila ombi la dhati hupata majibu. Jibu linaweza lisije katika namna ambayo unaipenda, au kwa wakati ambao unalitegemea; lakini litakuja kwa njia na kwa wakati ambao litakidhi mahitaji yako. Maombi unayofanya peke yako, ukiwa umechoka, ukiwa majaribuni, Mungu anayajibu, siyo daima kulingana na matarajio yako, lakini daima kwa ajili ya maslahi yako" (*Messages to Young Peo*ple, uk. 250).

Tunapojinyenyekeza na kuwasilisha hitaji letu, kwa njia iliyo wazi, dhahiri, tukikiri utegemezi wetu kamili kwa Mungu, Yeye hujibu. Hata hivyo, mara nyingi tunapaswa kusubiri. Mara nyingi tunahitaji kutumia uwezo na chaguzi zetu zote kabla ya Mungu kuingilia kati, ili tuweze kujua kwa uhakika kwamba alikuwa ni Yeye.

Kama Yeye angelijibu mara moja, tungaliweza kuchukua sifa kwa ajili yetu wenyewe.

Tunapoona hakuna njia iwezekanayo ya kutatua mgogoro, Mungu husema neno, na jambo ambalo hatukuweza kuwaza linatokea. “Niite, nami nitakuitikia, nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua” (Yer. 33:3).

Hata hivyo, ikiwa Mungu hatajibu kwa wakati huo na kwa njia tuombayo, tunaweza kufikiri kwamba hakujibu kabisa. Mungu hujibu maombi ya dhati, ya unyenyekevu na jibu Lake ndilo jibu bora zaidi.

Umeitwa ili kuujua upendo wa Mungu (Efe. 3:19). Hiyo ndiyo yote unayohitaji. Kadiri unavyomjua zaidi, ndivyo unavyomwamini zaidi, ndivyo unavyokuwa na amani zaidi na ndivyo unavyokuwa tayari kungoja uongozi Wake na kuingilia kati Kwake. Kaza macho yako Kwake, katika upendo Wake, ahadi Zake na kwa njia ambayo Ameongoza katika changamoto zilizopita.

“Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea” (Isa. 26:3).

Mungu anaujua wakati ujao. Anakujali, lakini pia anawajali wengine. Anaweza asijibu sasa kwa sababu Analo jibu bora zaidi au si wakati mzuri zaidi, au hauko tayari kwa mpango Wake. Anaweza kuwa na jibu tofauti ambalo linashughulikia mahitaji mengine, mambo ambayo huwezi kuyafikiria. Anaweza pia kuruhusu kitu fulani maishani mwako kama njia pekee ya kumfikia mtu ambaye vinginevyo hangefikiwa. Mambo mengi yanatokea ambayo tutayaelewa mbinguni tu.

Zingatia kwamba, Yesu hakuja na kufa ili kutupatia maisha ya starehe duniani. Kwa kweli, alisema kwamba katika ulimwengu huu tutapata majaribu (Yohana 16:33). Mara nyingi hutumia majaribu ili kutufundisha masomo muhimu kwa ajili ya ukuaji wa tabia na wokovu. “Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana” (2 Kor. 4:17).

Kwa hiyo badala ya kumwomba Mungu ili aondoe changamoto, mwombe Yeye ili akusaidie kukua na kujifunza kupitia hizo. Hitaji letu kuu zaidi si mahitaji tuyaombayo, japokuwa mara nyingi ni mahitaji halisi. Hitaji letu kuu ni kumjua Mungu wetu. Kadiri unavyomjua zaidi, ndivyo unavyomwamini zaidi na ndivyo unavyomruhusu zaidi kufanya kazi.

Mungu anakuita kuomba na kumtafuta Yeye, tafuta uwepo Wake, mpango Wake, uongozi Wake. Tafuta kumjua kabla ya kutafuta majibu na msaada, kisha telekeza juu Yake wasiwasi wako wote na umngoje Bwana.

Hebu na Tuombe Pamoja

**Muda wa Maombi (Dakika 30–45)**

*Vikundi vyote vya maombi vina njia tofauti za kuomba pamoja. Tunawahimiza kutumia dakika 30-45 zinazofuata katika maombi ya pamoja, kwa njia yoyote ambayo Roho Mtakatifu anaongoza. Tunahimiza maombi mafupi ya wazi (sentensi 1-3). Hii inaruhusu watu wengi zaidi kuomba mara nyingi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya kuomba kupitia Maandiko kulingana na mada. Unaweza kuomba kupitia vifungu vingine pia na kujumuisha masomo mengine katika wakati wako wa maombi. Tazama Mwongozo wa Kiongozi na Maombi ya Maombi ya Kanisa Ulimwenguni kwa mawazo ya maombi.*

**Kuomba Sawasawa na Neno la Mungu—Isa. 40:31a**

“Bali wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya”

**“Wao Wamngojeao Bwana”**

*Baba, huwa hatupendi kungojea. Kungoja hutufanya tuwe na wasiwasi na woga, kwa hiyo kwa haraka tunasonga mbele na kutafuta suluhu zetu wenyewe. Utufundishe kutulia ndani yako kama vile mtoto apumzikavyo mikononi mwa baba yake. Tupe imani ya kujua kwamba unaishikilia kesho katika mikono Yako yenye nguvu. Tuweze kuishi kwa imani, si kwa kuona.*

## "Watapata Nguvu Mpya"

*Bwana, wakati mwingine tunachoshwa na maisha katika ulimwengu huu usio na matumaini. Tumechoshwa na magonjwa, kutoelewana, umaskini, ukosefu wa haki, na upweke. Tafadhali inua macho yetu mbinguni na ufanye upya nguvu zetu. Tufundishe kukutegemea Wewe na kupata nguvu katika ahadi Zako zisizo na mwisho. Tunapokuwa dhaifu, tuunganishe na uwezo Wako.*

## Mapendekezo ya Maombi Zaidi

**Shukrani na Sifa:** Shukuruni kwa baraka mahususi na Msifuni Mungu kwa wema Wake.

**Kuungama:** Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

**Uongozi:** Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

**Kanisa Letu:** Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

**Mahitaji ya Eneo Mahalia:** Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

**Sikiliza na Uitike:** Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

## Mapendekezo ya Nyimbo

- Furaha Gani (Vk. 251 & Vd. 43)
- Ni Salama Rohoni (Vk. 327 & Vd. 127)

Siku ya 05

# Jina Lako Litukuzwe

**Fungu Elekezi:** *"Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni"* (Mathayo 5:16).

**Sisi ni Barua ya Wazi**

Wakati fulani washiriki wa kanisa, pamoja na mchungaji, walijaribu kualika majirani kwenye baadhi ya matukio. Baadhi yao walikataa. Mchungaji aliuliza familia kadhaa alizokuwa akifahamiana nao kwa nini hawakutaka kuja. Kwa maneno tofauti wote walisema, "Ikiwa Ndugu __________ ni mshiriki hapo, ni bora tusije. Si mtu mwema wala hana upendo. Hana heshima wala aibu. Ni mdanganyifu, huwatendea vibaya wanyama wake wa nyumbani na ni mwenye hasira na mkorofi siku zote." Washiriki wengi wanamsikitikia tu.

Sala ya Bwana inaanza na maneno, "Baba yetu uliye mbinguni." Mungu si Mungu tu wa ulimwengu bali pia Anao uhusiano wa karibu na wa kina pamoja nasi. Kisha inaendelea, "jina Lako litukuzwe." Neno la Kiyunani si *hagios—likimaanisha* "takatifu, tukufu, enye kustahili heshima"—bali *hagiazo*—likimaanisha "kutakasa." Tunawezaje kumtakasa au kumfanya Mungu kuwa Mtakatifu wakati Yeye *ni* Mtakatifu?

Paulo anasema sisi ni barua inayosomwa na watu wote (2 Kor. 3:2). Katika 1 Wakorintho 4:9 anaandika, "kwa sababu tumekuwa tamasha kwa dunia."

Watu hawamwoni Mungu, wanatuona sisi. Mwenendo wetu wa kila siku unaweza kuwa wa kumtukuza Mungu na kumheshimu au unaweza kudhalilisha jina Lake na kuliwakilisha vibaya kanisa na kuleta athari mbaya kwa kazi Yake (Mt. 5:13–16).

Ingia katika uwepo wa Mungu kwa nyimbo za sifa na kisha umtambue kuwa ni Baba yako mpendwa. Badala ya kujizingatia wewe na mahitaji yako, kwanza mzingatie Mungu, tunza sana jina Lake na heshima Yake. Mungu angependa tuombe kwa ajili ya vitu vile ambavyo vitaleta heshima kwa jina Lake. Hatupaswi kamwe kujitukuza wenyewe; tunalazimika kumwomba Mungu kwa ajili ya neema na Baraka za kiroho, ili kwamba tuweze kulitukuza jina Lake katika tabia zetu. Mungu anahimidiwa, jina Lake linatukuzwa, pale watoto Wake wanapotoa katika maisha yao mwonekano wa tabia ya Yesu" (Manuscript 34, 1903, par. 15).

Omba jambo kama hili: "Baba, niwezeshe kukuheshimu katika yote nifanyayo leo. Niwezeshe kukuwakilisha vyema na kulibeba jina Lako ili kwamba watu wanaponiona wapate kukuimbia Wewe sifa. Niruhusu nitende kwa namna ambayo itawafanya watu kuona tabia ya Yesu katika matendo na maneno yangu yote."

Pia, katika maombi yako taka tu mambo ambayo yatamletea Mungu heshima na kumfurahisha. 1 Yohana 5:14 inasema kwamba, "tukiomba kitu sawasawa na mapenzi Yake, Atusikia."

Lazima tuombe katika Jina la Yesu, lakini hiyo ina maana kubwa zaidi ya kusema tu "katika Jina la Yesu." Katika nyakati za Biblia, jina liliwakilisha tabia. Kuomba katika jina la Yesu ni kuomba kwa kuongozwa na mapenzi Yake, kuomba mambo ambayo yatamwakilisha Yeye na tabia Yake. Yakobo 4:3 anasema, "Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu." "Kuomba katika jina ya Yesu kuna maana sana. Kuna maana kwamba tunapaswa kuikubali tabia Yake, kumdhihirisha Roho Wake na kutenda kazi Zake" (Tumaini, seh. ya 2, uk. 280).

Yesu aliahidi kujibu maombi yetu ikiwa tunaomba katika Jina Lake, chini ya mapenzi Yake, na kwa ajili ya kitu ambacho kitamletea Mungu utukufu na heshima (Yohana 14:13, 14; 1 Yohana 5:14).

Na pale Mungu anapojibu maombi, hakikisha unamtukuza na kumhimidi Yeye. Hatupaswi kamwe kujichukulia utukufu sisi wenyewe. Shetani anajaribu kuuchukua utukufu wa Mungu kwa ajili yake mwenyewe. Kwa unyenyekevu, kwa moyo wa shukrani mkiri na kumtukuza Mungu kupitia maneno, matendo na maombi.

Tunapolalamika tunatoa ujumbe mbaya kumhusu Mungu wetu. Kwa namna hiyo tunasema kwamba Mungu si mwema, hajali, wala si mwaminifu kwa ahadi Zake. Furahini siku zote (1 Thes. 5:16; Fil. 4:4). Omba, nena na utende kwa namna ambayo itamletea heshima Mungu. Unawezaje kuamsha imani unapokuwa na mashaka? Unawezaje kuwataka watu wengine wamtukuze Mungu wakati wewe ni mwenye manung'uniko?

Maombi yetu ya dhati yanapaswa kuwa, "Baba yangu mpendwa wa mbinguni, ninaomba uniwezeshe kusema na kutenda kwa namna ambayo itakuwakilisha Wewe kikamilifu kwa wengine. Ninaomba unipatie tu yale mambo ambayo yatakuletea Wewe utukufu na unisaidie kuyatumia kwa namna ambayo itakuletea heshima. Niruhusu nilitukuze jina Lako leo."

**Muda wa Maombi (Dakika 30–45)**

*Vikundi vyote vya maombi vina njia tofauti za kuomba pamoja. Tunawahimiza kutumia dakika 30-45 zinazofuata katika maombi ya pamoja, kwa njia yoyote ambayo Roho Mtakatifu anaongoza. Tunahimiza maombi mafupi ya wazi (sentensi 1-3). Hii inaruhusu watu wengi zaidi kuomba mara nyingi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya kuomba kupitia Maandiko kulingana na mada. Unaweza kuomba kupitia aya nyingine pia na kujumuisha masomo mengine katika wakati wako wa maombi. Tazama Mwongozo wa Kiongozi na Maombi ya Maombi ya Kanisa Ulimwenguni kwa mawazo ya maombi.*

**Kuomba Sawasawa na Neno la Mungu—Mathayo 5:16.**

*“Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.”*

**“Nuru Yenu na Iangaze”**

*Bwana, Wewe ni chanzo cha nuru. Angaza kutokea ndani yetu ili wengine waweze kuona uzuri wa tabia Yako. Tuwezeshe kung’aa kwa mng’ao angavu na kwa ujasiri ili wengine wavutwe kwenye ufalme Wako kupitia upendo wetu.*

**“Wapate Kuyaona Matendo Yenu Mema”**

*Mungu wetu, mara nyingi tunasahau kwamba watu wengine wanatazama kila kitu tufanyacho. Wasaidie kuona upendo, siyo chuki maishani mwetu. Wasaidie kuona ukarimu si ubinafsi. Tenda maishani mwetu ili kuwabariki watoto wetu, jirani zetu na hata adui zetu.*

**“Wamtukuze BABA Yenu Aliye Mbinguni”**

*Mungu wetu, lazima wewe uongezeke na sisi tupungue. Tunyenyekeze na uwasaidie jirani zetu kuona nguvu na huruma Yako katika matendo yetu ya upendo.*

**Mapendekezo ya Maombi Zaidi**

**Shukrani na Sifa:** Shukuruni kwa baraka mahususi na Msifuni Mungu kwa wema Wake.

**Kuungama:** Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

**Uongozi:** Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

**Kanisa Letu:** Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

**Mahitaji ya Eneo Mahalia:** Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

**Sikiliza na Uitike:** Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

**Mapendekezo ya Nyimbo**

- Bwana Mungu (Vk. 28 )
- Nasifu Shani ya Mungu (Vk. 26 & Vd. 38)
- Mwumbaji, Mfalme (Vk. 7 & Vd. 9)

Siku ya 06

# Ufalme Wako Uje

**Fungu Elekezi:** *"Ufalme wa Mungu umo ndani yenu"* (Luka 17:21b).

**Wokovu Umeingia**

Katika Luka 19 anajitolea kuingia katika nyumba ya Zakayo. Kisha Yesu anasema, "Leo wokovu umefika nyumbani humu" (aya ya 9). Yesu anapoishi nyumbani mwako, mbingu yote iko hapo. Na kabla hujauingia ufalme wa Mungu, lazima ufalme wa Mungu uingie moyoni mwako. Katika Yohana 17 Yesu hakuomba kwamba wafuasi Wake waondolewe kimwili kutoka ulimwenguni bali kwamba wasiwe wa ulimwengu (Yohana 17:15, 16).

Lazima tuzoee kuishi hapa leo kama ambavyo tutaishi mbinguni. Ikiwa tunajikita kwa mambo ya ulimwengu, tutakuwa kama ulimwengu. "Hazina yako ilipo, ndipo na moyo wako utakapokuwapo" (Mt. 6:21). Lakini kama tukijikita kwa Mungu na kwenye ufalme Wake, ufalme Wake utakuwa ndani yetu na karibu nasi. "Nyuso za wanaume na wanawake wanaozungumza na Mungu, ambaye ulimwengu usioonekana ni halisi kwao, huonesha amani ya Mungu. Wanabeba pamoja nao angahewa la mbinguni kunjufu na la kupendeza" (*Medical Ministry,* uk. 252).

Kwenye safari moja ya kiuinjilisti nchini Kuba, watoto wengi pamoja na wazazi wao walikuja kusikiliza. Nilifahamu kutoka kwa mchungaji kwamba wageni hawa wote walikuja kwa sababu ya mwanamke mmoja. Nilimwuliza ni nini alichokisema ili kuwafanya waje. Akanijibu, "siyo kile nilichowaambia," na kisha akatualika tumtembelee siku iliyofuata na kuangalia. Kwa hiyo tulienda.

Alikuwa na nyumba ndogo sana, kama kibanda cha kutunzia vifaa. Hakukuwa na samani ndani isipokuwa vitanda viwili vya dabodeka, meza

ndogo, viti viwili vidogo na jiko la kukambikia. Mapema mchana alitoka nje mbele ya nyumba yake. Na kisha wakaja—takribani watoto mia mbili! Aliwaketisha chini mavumbini na kumwonesha karatasi zilizosainiwa na wazazi wao. Kisha watoto walipanga msitari na akawagawia wali wote. Wakaketi chini na kula.

Walipokuwa wanakula, alitueleza kwamba jirani zake wengi hawakuwa na ajira, lakini alikuwa amebarikiwa kuwa nayo. Mshahara wake usingetosha kununua vyakula vya aina mbalimbali, bali aliweza kununua mchele. Na kisha akasema, "Tumeitwa kuwa kama Yesu, ili kuonesha jinsi ulivyo ufalme wa Mungu kwa hiyo watu wanauhitaji. Tunapaswa kutumia mbinu ya Yesu. Kuwalisha na kujenga urafiki. Ikiwa ninaishi kwa ajili yangu, ninakuwaje kama Yesu? Na ikiwa ninawapa tu watu mkate wa kimwili, unawezaje kuwasaidia? Kwa hiyo ninatumia ubwabwa ili kuwaonesha watoto upendo. Kisha ninawapa pia mkate wa kiroho. Lakini watoto mara nyingi huhamishwa mawazo yao. Ili kuhakikisha kwamba watoto wanasikiliza, lazima waende nyumbani na, kama uthibitisho kwamba walizingatia, wawaambie wazazi wao kisa na wimbo waliojifunza leo. Kwa njia hii ninawafikia pia wazazi wao. Sasa kwa sababu nimekuwa nikifanya hivi kwa muda, wote wananipenda, wananiamini na wako tayari kusikiliza."

Punde tu watoto walipomaliza kula, alianza kuwafundisha kuhusu Yona na kisha aliwafundisha wimbo. Baada ya hapo, walimkumbatia na kumshukuru. Niliwasikia wakisema, "Tunakupenda mama!" Alikuwa na tabasamu kubwa usoni mwake. Akasema, "Siyo hivyo tu kwamba ninajaribu kuwaonesha ufalme wa Mungu, lakini pia wananibariki na kunijaza furaha pia. Furaha yangu kubwa ni kuwaona wakija kanisani na kuomba na kumjifunza Mungu. Lakini furaha yangu kuu zaidi itakuwa ni kuwaona mbinguni. Kwa hiyo ninataka wapate muonjo kidogo wa mbinguni sasa."

Yesu anakuja hivi karibuni! Lakini kwa wewe kuwa tayari kuuingia ufalme Wake pale atakapokuja, lazima uwe na ufalme Wake ukiishi

ndani yako sasa. Lazima uombe kila siku, “Bwana, naomba uje na ufalme Wako ndani ya moyo wangu leo.” Mungu anakuita kuufanya ufalme Wake kuwa halisi leo. Kwa njia ya maombi, usomaji wa Neno la Mungu na huduma ya furaha, ishi hapa kama utakavyo kuishi mbinguni. Iruhusu mbingu ikae ndani yako. Kuwa mkono wa Mungu hapa, kama ambavyo watu wa Imani walikuwa mikono Yake hapo kale.

Mungu anataka kuhamishia ufalme Wake moyoni na nyumbani mwako leo na kila siku. Anakutaka uzoee kuishi katika uwepo Wake kama raia wa mbinguni. Kila siku ialike mbingu ndani ya moyo wako na kuruhusu upendo Wake umwagike kwa wengine kupitia matendo yako.

Hebu Tuombe Pamoja

**Muda wa Maombi (Dakika 30–45)**

*Vikundi vyote vya maombi vina njia tofauti za kuomba pamoja. Tunawahimiza kutumia dakika 30-45 zinazofuata katika maombi ya pamoja, kwa njia yo yote ambayo Roho Mtakatifu anaongoza. Tunahimiza maombi mafupi ya wazi (sentensi 1-3). Hii inaruhusu watu wengi zaidi kuomba mara nyingi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya kuomba kupitia Maandiko kulingana na mada. Unaweza kuomba kupitia vifungu vingine pia na kujumuisha masomo mengine katika wakati wako wa maombi. Tazama Mwongozo wa Kiongozi na Maombi ya Maombi ya Kanisa Ulimwenguni kwa mawazo ya maombi.*

**Kuomba Sawasawa na Neno la Mungu—Luka 17:21b**

*“Ufalme wa Mungu umo ndani yenu”*

**“Ufalme wa Mungu”**

*Bwana, tunajua ufalme Wako si juu ya mamlaka au nguvu za ulimwengu. Utupe hekima ya kuelewa na kuuishi ufalme wako mtulivu katika maisha yetu leo. Tukamilishe ili tutumike, ili tufariji, na kuwatia moyo watoto Wako wa duniani.*

**"Umo Ndani Yenu"**

*Baba Mungu, tunaomba utusaidie kuishi kama raia wa mbinguni kuanzia leo. Geuza macho yetu kutoka kwetu ili tuwaangalie wengine. Ni mtu gani karibu nasi anahitaji sikio la kumsikiliza hivi sasa? Nani anahitaji chakula cha ukarimu au nguo kwa ajili ya watoto wao? Nani anahitaji kusikia ushuhuda wetu kuhusu nguvu ya Yesu inayobadilisha? Zungumza na mioyo yetu na usimamishe ufalme Wako katika maisha yetu leo.*

**Mapendekezo ya Maombi Zaidi**

**Shukrani na Sifa:** Shukuruni kwa baraka mahususi na Msifuni Mungu kwa wema Wake.

**Kuungama:** Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

**Uongozi:** Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

**Kanisa Letu:** Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

**Mahitaji ya Eneo Mahalia:** Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

**Sikiliza na Uitike:** Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

**Mapendekezo ya Nyimbo**

- Tawala ndani Yangu (Vk. 339 & Vd. 147)
- Yu Hai, Yu Hai (Vk. 93 & Vd. 167)

Siku ya 07

## Mapenzi Yako Yatimizwe Hapa Duniani Kama Huko Mbinguni

**Fungu Elekezi:** *"Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho"* (Yeremia 29:11).

**Yeye ni Bwana**

Wote tunayo mipango, ya muda mrefu na ya kila siku. Katika maombi *yetu* mara nyingi tunamwomba Mungu kusaidia na kubariki mipango yetu badala ya kutafuta mipango ya *Mungu*. Mungu anasema, "Nayajua mawazo ninayowawazia ninyi" (Yeremia 29:11). Ili kupata baraka na uwezo wa Mungu, lazima ufuate mpango Wake.

Katika maombi tunamwagiza Mungu kufanya kana kwamba sisi ni bwana na Yeye ni mtumwa. Kumbuka kuwa, Yeye ni Mungu, Yeye ni Bwana. Anapaswa kutuagiza nini cha kufanya. Kila siku jiweke wakfu kwa Mungu kwa ajili ya siku hiyo. Salimisha mipango yako yote Kwake, ili itimilizwe au ili itolewe kama ambavyo mapenzi Yake yataonesha. Ndivyo ambavyo siku kwa siku utakuwa ukiyatoa maisha yako kwenye mikono ya Mungu" (*Steps to Christ*, uk. 70).

Kumbuka usemi huu katika sala ya Bwana: "Mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama huko mbinguni." Huko mbinguni malaika wanamtumikia Mungu. Anawapatia kazi ya kufanya, nao wanaifanya. Jibu lao ni hili, "Ndiyo, Bwana," na kisha wanaenda kufanya. Hakuna hata mmoja wao anayemwambia Mungu nini cha kufanya; hakuna anayehoji au kusema, "nina kazi nyingi" au "nitaifanya baadaye." Hakuna anayelalama kwa kusema, "Sina uwezo" au Ninalo wazo jema zaidi." Anapomwambia malaika kufanya kitu, wanafanya, wakijua kwamba Yeye anatoa uweza wote muhimu wanaouhitaji.

Siku moja mimi na mke wangu tulikuwa na safari ya kuendesha kwa saa kumi na moja. Kama kawaida, tuliomba mpango wa Mungu kwa ajili ya siku hiyo na kumwomba Yeye atuoneshe fursa za kutumika. Takribani saa tano baadaye tukiwa safarini, mchungaji rafiki mwema alinipigia simu. "Niombee," alisema. Ninapaswa kwenda Kuba kwa ajili ya uinjilisti, lakini gari langu limeharibika na basi halikuja."

Nilijua kuwa alikuwa akiishi katika eneo tulikokuwa tunapita wakati huo, kwa hiyo nilisema, "kwani unaishi wapi katika eneo hili?" Alinielekeza pa kuingilia. Tulipokuwa bado tunaongea, nilifika mahali pa kuingilia. "Tumefika hapa!" Nilisema kwa mshangao. "Inawezekanaje?" aliuliza. "Unaishi umbali wa kuendesha gari kwa saa tano kutoka kwangu upande wa kaskazini!" Tulifuata njia ile, tukafika nyumbani kwake, tukamchukua na kumpeleka mpaka uwanja wa ndege. Akapanda ndege na kwenda zake Kuba!

Mara nyingi tumeendelea kujitahidi na kushindwa katika juhudi zetu kwa sababu tunatenda kwa mipango yetu wenyewe. Lakini, hatujui vizuri kila kitu. Hatujui yajayo. Mungu anajua na Anatupenda.

"Wengi sana, katika kupanga kwa ajili ya siku njema zijazo, hushindwa kabisa. Mruhusu Mungu akupangie…. Mungu kamwe hawaongozi watoto Wake kinyume na vile ambavyo wangechagua kuongozwa, kama wangeweza kuona mwisho tangu mwanzo na kutambua utukufu wa kusudi wanalolitimiza kama watendakazi pamoja na Yeye" (*The Ministry of Healing*, uk. 479).

Ili kuyafanya mapenzi ya Mungu ni lazima uyafahamu, kwa hiyo unapaswa pia kusikiliza uwapo katika maombi. Kile Mungu anachokuambia ni muhimu zaidi kuliko kile unachomweleza. Sisi "tunapaswa kuwa na uzoefu binafsi katika kupata kujua mapenzi ya Mungu. Tunalazimika kila mmoja kumsikia Yeye akizungumza moyoni. Wakati kila sauti imenyamazishwa na katika ukimya tunamngoja Yeye, ukimya wa roho unaifanya sauti ya Mungu kusikika vizuri" (*The Ministry of Healing*, uk. 58).

Kwa njia ya maombi tunazungumza na Mungu, na kwa njia ya Neno Mungu anasema nasi. Maombi na usomaji wa Neno daima huenda pamoja; kamwe havipaswi kutenganishwa. Biblia ni sauti ya Mungu akisema nasi, dhahiri tu kama vile ambavyo tungeisikiliza kwa masikio yetu" (*Testimonies for the Church*, vol. 6, uk. 393).

Kwa hakika tunaweza kumwambia Yeye mahitaji yetu. Tunaambiwa kuweka mahitaji yetu yote juu Yake (1 Petro 5:7). Hakuna kosa lolote katika kumwomba msaada. Hata hivyo, haumjulishi Mungu kuhusu jambo ambalo bado halijui; badala yake, unampatia Yeye ukubali wako ili akusaidie. Mungu alitupatia uhuru wa kuchagua na anaheshimu chaguzi zetu. Kamwe hataingilia kati kwa kulazimisha mapenzi Yake kwetu. Anatusubiria mpaka pale tunapoomba, tunapochagua msaada Wake na kisha huingilia kati.

Omba, soma Neno, litafakari Neno. Wasilisha mahitaji na mipango yako na uombe kwa ajili ya maelekezo na mwongozo. Ifanye mipango ya Mungu kuwa kipaumbele chako. Mtafute Mungu kwanza, kisha uamini kwamba atakupatia mahitaji yako yote kama alivyoahidi (Mt. 6:33). Kuwa tayari kumtumikia na kufuata mapenzi Yake. Sema, "Mimi hapa Bwana. Unitumie leo. Mapenzi Yako yatimizwe katika maisha yangu leo."

Hebu Tuombe Pamoja

**Muda wa Maombi (Dakika 30 – 45)**

***V**ikundi vyote vya maombi vina njia tofauti za kuomba pamoja. Tunawahimiza kutumia dakika 30-45 zinazofuata katika maombi ya pamoja, kwa njia yo yote ambayo Roho Mtakatifu anaongoza. Tunahimiza maombi mafupi ya wazi (sentensi 1-3). Hii inaruhusu watu wengi zaidi kuomba mara nyingi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya kuomba kupitia Maandiko kulingana na mada. Unaweza kuomba kupitia vifungu vingine pia na kujumuisha masomo mengine katika wakati wako wa maombi.*

*Tazama Mwongozo wa Kiongozi na Maombi ya Maombi ya Kanisa Ulimwenguni kwa mawazo ya maombi.*

**Kuomba Sawasawa na Neno la Mungu—Yeremia 29:11.**

*"Kwa  kuwa Nayajua mawazo ninayowawazia ninyi…. Ya kuwapa tumaini siku zenu za Mwisho."*

**"Maana Nayajua Mawazo Ninayowawazia Ninyi"**

*Bwana, tunajishughulisha sana na mawazo yetu wenyewe. Tunaomba Utusamehe kwa tamaa, uchoyo na ubinafsi. Badala yake, tuoneshe mipango Yako. Elekeza macho yetu kuona mahitaji yanayotuzunguka. Fanya mikono na miguu yetu iwe tayari kutumika.*

**"Mawazo ya Kuwapa Tumaini Siku za Mwisho"**

*Baba Mungu, mipango yetu ya kidunia itasambaratika na kubatilika, lakini mipango Yako inadumu hata umilele. Asante kwamba kushindwa kwetu siyo kwa kudumu. Tupe imani ya kuutazama ufalme Wako leo. Ishi maisha Yako ndani yetu.*

**Mapendekezo ya Maombi Zaidi**

**Shukrani na Sifa:** Shukuruni kwa baraka mahususi na Msifuni Mungu kwa wema Wake.

**Kuungama:** Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

**Uongozi:** Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

**Kanisa Letu:** Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

**Mahitaji ya Eneo Mahalia:** Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

**Sikiliza na Uitike:** Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

**Mapendekezo ya Nyimbo**

- Yote Namtolea Yesu (Vk. 332 & Vd. 122)
- Twae Wangu Uzima (Vk. 163 & Vd. 146)

Siku ya 08

## Utupe Leo Riziki Yetu

**Fungu Elekezi:** *"Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho. Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na hasa jamaa ya waaminio"* (Gal. 6:9, 10).

**Mungu Atatoa**

Siku moja nilitumia muda kushughulikia mipango inayohusiana na fedha. Baada ya kutenga zaka yetu na asilimia ndogo kwa ajili ya utume na wahitaji, nililipa bili zote, nikatenga baadhi kwa ajili ya karo ya shule ya vijana wetu na kuwa na sehemu ndogo iliyobaki kwa muda uliobaki wa mwezi kwa ajili ya chakula na gharama nyinginezo. Niliingia kwenye gari letu ili nipeleke fedha za karo hadi shuleni na kuondoka. Mvua kubwa ilikuwa ikinyesha.

Kabla tu ya kuingia kwenye barabara kuu ya shule, nilimwona mwanamama mmoja akionekana kuwa na huzuni. Nilisimamisha gari na kugundua kuwa ni mwanamama ambaye nilikuwa nimembatiza miezi michache tu iliyokuwa imepita. Alikuwa akilia.

"Kuna tatizo gani?" niliuliza. Hatimaye alieleza kwamba yeye, pamoja na wengine wengi, alikuwa amepoteza kazi wakati kiwanda cha jirani kilipofungwa. Kisha yeye, pamoja na watoto wake wawili wadogo, alifukuzwa katika nyumba yake kwa kuwa hakuweza kulipa kodi. Na sasa hawakuwa na chakula tena.

Nilimpeleka kwenye duka la vyakula na kujaza chakula kwenye mkokoteni, nikilipa kwa kutumia sehemu ya karo ya shule. Katika kumrudisha shuleni, nilimpigia simu mwenye nyumba na kwa shida nilifanikiwa kufanya makubaliano naye ambapo nilitumia fedha ya karo

iliyobaki kulipa nusu ya deni lake na mwenye nyumba alisamehe nusu nyingine. Niliwapigia simu wajumbe wa baraza la kanisa na walilipa bili ya umeme. "Pia," nikasema, "baada ya kusimama, msaidie mtu mwingine aliye na uhitaji." Alishukuru sana.

Nilipofika nyumbani na kumwambia mke wangu kwamba nilikuwa nawaza jinsi tutakavyolipa karo, alisema kwa shangwe, "Mungu atatoa." Mchana ule nilipoangalia sanduku la barua, nilipata bahasha yenye hundi ndani yake. Ni kiasi kile kile nilichotumia kumsaidia yule mwanamama.

Mungu anatujali sana zaidi ya vile tunavyowajali watoto wetu. Anaahidi kwamba atatulisha (Isa. 33:16). Lakini zingatia neno *utupe* kwenye aya: "utupe leo riziki yetu." Kwa uwazi kabisa Yesu anatudokeza kwamba tusiombe tu kwa ajili yetu bali pia kwa ajili ya wale wanaotuzunguka. Kwa kweli, Biblia iko wazi kabisa kwamba sharti tuwapende wengine kama vile tunavyojipenda (Marko 12:31), na lazima tuombe kwa ajili ya wengine (Yakobo 5:16). "Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo" (Gal. 6:2). Wanafunzi wa karne ya kwanza walifanya hivyo. Walikuwa wamoja katika kila kitu walichokifanya (Matendo 4:32).

"Sala zetu hazipaswi kuwa ombi la ubinafsi, kwa faida yetu wenyewe. Tunapaswa kuomba ili tuweze kutoa. Kanuni ya maisha ya Kristo lazima iwe kanuni ya maisha yetu.... Tunapaswa kuomba baraka kutoka kwa Mungu ambazo tunaweza kuzifikisha kwa wengine. Uwezo wa kupokea hupokelewa tu kwa kutoa. Hatuwezi kuendelea kupokea hazina za mbinguni bila kuziwakilisha kwa wale wanaotuzunguka" (*Christ's Object Lessons*, uk. 142, 143).

Zingatia kwamba sala ya Bwana haizungumzi kuhusu riziki kwa ajili ya kesho, ni kwa ajili ya leo tu. Wana wa Israeli waliweza kuokota mana kwa ajili ya siku moja tu (Kut. 16:4). Mungu hataki usumbukie ya kesho (Mt. 6:34). Omba kwa ajili ya leo. Omba ili uwasaidie wengine. Tafuta kuwabariki. Kabla wafuasi wa Yesu hawajahubiri, wanapaswa kuonesha upendo wao kwa Mungu kwa kuwa mbaraka kwa wale wanaowazunguka.

Katika hukumu Yesu hatauliza kama ulienda kanisani au ulifanya mambo mengine mazuri, ingawa hatupaswi kuacha kukusanyika(Ebr. 10:25). Atasema, "Nalikuwa ni uchi na mwenye njaa na kiu. Jinsi ulivyowapenda wale waliokuzunguka inaonesha jinsi ulivyonipenda" (tazama Mt. 25:31–45).

Mungu anakuita ili uombe kwa ajili ya jirani yako, mpende jirani yako na uwe mbaraka kwa wote wanaokuzunguka.

Hebu Tuombe Pamoja

**Muda wa Maombi (Dakika 30–45)**

*Vikundi vyote vya maombi vina njia tofauti za kuomba pamoja. Tunawahimiza kutumia dakika 30-45 zinazofuata katika maombi ya pamoja, kwa njia yo yote ambayo Roho Mtakatifu anaongoza. Tunahimiza maombi mafupi ya wazi (sentensi 1-3). Hii inaruhusu watu wengi zaidi kuomba mara nyingi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya kuomba kupitia Maandiko kulingana na mada. Unaweza kuomba kupitia vifungu vingine pia na kujumuisha masomo mengine katika wakati wako wa maombi. Tazama Mwongozo wa Kiongozi na Maombi ya Maombi ya Kanisa Ulimwenguni kwa mawazo ya maombi.*

**Kuomba Sawasawa na Neno la Mungu—Wagalatia 6:9, 10.**

*"Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho. Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na hasa jamaa ya waaminio."*

**"Hebu Tusichoke katika Kutenda Mema"**

*Baba, wakati mwingine huduma hutuacha tukiwa tumechoka. Tunazingatia sana mipango na matokeo na kusahau kuwa Wewe ndiye Chanzo cha nguvu zote. Tafadhali elekeza macho yetu kwako. Ufufue roho zetu na utujaze na upendo Wako usioisha kwa ulimwengu wenye uhitaji.*

**"Tutavuna kwa Wakati Wake, Tusipozimia Roho"**

*Bwana, asante kwa ahadi hii kwamba siku ya mavuno inakuja. Ifanye mikono yetu kuwa ya uaminifu tunapopanda na kumwagilia mbegu za imani kwa wengine. Matokeo ni juu yako!*

**"Tuwatendee Watu Wote Mema"**

*Mungu wetu, tunaomba utupatie macho ili tuone fursa kwa ajili ya huduma. Tuoneshe jinsi ambavyo tunaweza kuonesha upendo kwa watoto wetu, wenzi wetu, jirani zetu na kwa washiriki wenzetu kanisani. Tunafurahi sana kuwa sehemu ya familia ya Mungu!*

**Mapendekezo ya Maombi Zaidi**

**Shukrani na Sifa:** Shukuruni kwa baraka mahususi na Msifuni Mungu kwa wema Wake.

**Kuungama:** Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

**Uongozi:** Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

**Kanisa Letu:** Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

**Mahitaji ya Eneo Mahalia:** Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

**Sikiliza na Uitike:** Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

**Mapendekezo ya Nyimbo**

- Kuwatafuta Wasioweza (Vk. 195 & Vd. 100)
- Twapanda Mapema (Vk. 193 & Vd. 55)
- Walio Kifoni (Vk. 202 & Vd. 56)

Siku ya 09

## Utusamehe Deni Zetu kama Nasi Tuwasamehevyo Wadeni Wetu

**Fungu Elekezi:** *“Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi”* (Mt. 6:14).

**“Sikuuhisi”**

Alikuwa mzee na amekuwa mzee katika kanisa langu kwa miaka mingi. Kwa sasa alikuwa hospitalini. Nilipomtembelea, aliniambia, “Usiniombee, maana nimepotea.” “Kwa nini unasema hivyo?” nilimjibu. “Mchungaji, nimetenda dhambi. Nilifanya dhambi kubwa sana nilipokuwa kijana.” Je! Ulimwomba Mungu msamaha?” “Aa, naomba kila siku maishani mwangu, lakini kamwe hajanisamehe.” “Unawezaje kujua kuwa hajakusamehe?” “Naam,” alisema, sikuhisi kusamehewa.” Tuliongelea jambo hilo, mwisho wa mazungumzo yetu alikuwa na furaha na amani.

Unawezaje “kuuhisi” msamaha? Je! Ni hisia ya joto mwilini mwako au kitu cha baridi mikononi mwako, au mtekenyo nyuma ya shingo yako? Je! Unaweza kuunusa?

Biblia iko wazi. “Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote” (1 Yohana 1:9). Haisemi kuwa anasamehe dhambi ndogo tu au idadi fulani ya dhambi. Inasema wazi kwamba tukiziungama dhambi zetu, Hutusamehe ZOTE. Sharti ni kwamba: lazima utubu. Ahadi: Mungu anasamehe. Fanya sehemu yako na Mungu atafanya ya Kwake.

Msamaha si kitu ambacho unaweza kukihisi au kukithibitisha kisayansi. Ni kwa imani. Unalichukua Neno la Mungu kama lilivyo na kuamini kwamba Mungu hasemi uongo. Huwezi kuuelezea, hauustahili, lakini unajua kwamba Mungu aliahidi na ahadi Zake ni za hakika kwa asilimia

100 kwa sababu zinategemea tabia na Neno Lake. Hakuna kitu kilicho thabiti kuliko Neno la Mungu.

Unapoungama, mara moja unasamehewa. Yesu tayari alishalipa bei ya dhambi yako pale msalabani. Yeye ni "Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu" (Yohana 1:29). Damu Yake inatosha, na katika damu Yake mna ukombozi kwa ajili ya dhambi zenu zote (Efe. 1:7).

Baada ya kuungama unahitaji kuiweka Imani katika vitendo, ili kuchagua kuamini kwamba Mungu anafanya kile alichoahidi. "Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki" (Rum. 4:3). Kumbuka, "Mwenye haki ataishi kwa Imani" (Rum. 1:17). Unapoamini, Mungu anatenda, na unakuwa umesamehewa. Usijaribu kuuelezea au kudhani unaustahili. "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu" (Efe. 2:8).

Kupitia jambo hili rahisi la kumwamini Mungu, Roho Mtakatifu amezalisha maisha mapya moyoni mwako. Wewe ni kama mtoto aliyezaliwa kwenye familia ya Mungu na Anakupenda kama vile ampendavyo Mwanawe" (*Steps to Christ*, uk. 52). Msamaha, haki, wokovu—vyote vinapokelewa kama zawadi kwa imani.

"Wewe ni mwenye dhambi. Hauwezi kulipia fidia kwa ajili ya dhambi zako zilizopita; hauwezi kuubadili moyo wako na kujifanya kuwa mtakatifu. Lakini Mungu anaahidi kufanya haya yote kwa ajili yako kupitia kwa Yesu. Wewe *iamini* tu ile ahadi.... Ukiiamini ahadi ... Mungu anaweka ukweli.... Usingoje *kuhisi* kwamba umekamilishwa, bali sema, "ninaamini hivi, ndivyo ilivyo, si kwa sababu ninauhisi, bali kwa sababu Mungu ameahidi" (*Steps to Christ*, uk. 51).

Unapokaza macho yako kwenye msalaba wa Yesu, unapata taswira ya udhihirisho huo mkubwa wa upendo: Yesu, Mwumbaji, Yule anayetamka

na vinakuwa, Yule ambaye malaika hujifunika mbele Yake, Mungu wa Ulimwengu aliyeshuka na kuchukua umbo la mwanadamu. Yeye, Aliye Mtakatifu, alizichukua dhambi zako na kufa kwa ajili yako wewe binafsi. Mungu alikufa kwa ajili yako.

Kaza macho yako kwenye msalaba Wake. Kisha utagundua kwamba wale wanaopitia uzoefu wa neema pia huishiriki neema na wengine kwa ukarimu. Wale wanaopata msamaha, wanasamehe. Msingi wa msamaha wote unapatikana katika upendo wa Mungu tusioustahili, lakini kwa mtazamo wetu kwa wengine tunaonesha kama vile tumeufanya upendo huo kuwa wetu" (*Christ's Object Lessons*, uk. 251).

Hebu Tuombe Pamoja

**Muda wa Maombi (Dakika 30–45)**

*Vikundi vyote vya maombi vina njia tofauti za kuomba pamoja. Tunawahimiza kutumia dakika 30-45 zinazofuata katika maombi ya pamoja, kwa njia yo yote ambayo Roho Mtakatifu anaongoza. Tunahimiza maombi mafupi ya wazi (sentensi 1-3). Hii inaruhusu watu wengi zaidi kuomba mara nyingi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya kuomba kupitia Maandiko kulingana na mada. Unaweza kuomba kupitia vifungu vingine pia na kujumuisha masomo mengine katika wakati wako wa maombi. Tazama Mwongozo wa Kiongozi na Maombi ya Maombi ya Kanisa Ulimwenguni kwa mawazo ya maombi.*

**Kuomba Sawasawa na Neno la Mungu—Mathayo 6:14.**

*"Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi."*

**"Mkiwasamehe Watu Makosa Yao"**

*Baba, tunakiri kwamba wakati fulani hatutaki kusamehe. Tuweke huru kutoka katika uchungu na chuki. Badili mioyo yetu na uiruhusu neema*

*Yako itiririke kupitia kwetu hadi kwa wengine. Badilisha adui zetu kuwa marafiki na uunganishe mioyo yetu katika huduma kwa ajili ya ufalme Wako.*

**"Baba Yenu wa Mbinguni Atawasamehe Ninyi"**

*Asante Bwana, kwa zawadi tusizostahili za toba na ukombozi. Wakati mwingine tunahangaika kukubali msamaha Wako na kujaribu kupata kibali Chako. Tunaomba utufundishe kupokea msamaha Wako kwa furaha na kuieneza neema hiyo kwa wengine.*

**Mapendekezo ya Maombi Zaidi**

**Shukrani na Sifa:** Shukuruni kwa baraka mahususi na Msifuni Mungu kwa wema Wake.

**Kuungama:** Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

**Uongozi:** Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

**Kanisa Letu:** Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

**Mahitaji ya Eneo Mahalia:** Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

**Sikiliza na Uitike:** Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

**Mapendekezo ya Nyimbo**

- Nimekombolewa na Yesu (Vk. 178 & Vd. 35)
- Yesu Mwokozi (Vk. 248 & Vd. 51)

Siku ya 10

# Usitutie Majaribuni

**Fungu Elekezi:** *"Maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu mtu"* (Yakobo 1:13).

**Je! Mungu Anafanya Hivyo Kweli?**

Mungu ni mtakatifu, Yeye ni upendo. Hamjaribu mtu awaye yote, tunajitia wenyewe majaribuni (Yakobo 1:14, 15). Kwa hiyo sasa, umewahi kujiuliza kwamba Yesu alimaanisha nini aliposema katika Sala ya Bwana, "Usitutie majaribuni"? Yesu hakuwa anamaanisha kwamba Mungu hutujaribu mpaka tutende dhambi na kwamba ni lazima tumwombe ili asitusukumie majaribuni.

Kwa hiyo, ina maana gani? Kama ilivyo katika lugha nyingi kama siyo zote, maneno yanaweza kuwa na maana zaidi ya moja katika Kiyunani. Kwa hiyo ni lazima uangalie kwenye lugha ya asili na muktadha wake. Neno la Kiyunani "ongoza (tia)" ni *eisphero*. Aya hii inaweza kutafsiriwa kama "usituruhusu kwenda, usitutelekeze hapo, usitupatie ruhusa ya kwenda." Haimaanishi "kushawishi."

Neno la Kiyunani kwa "majaribu" ni *peirasmon*. Linaweza kufasiriwa kama "jaribio, tahini, taabu," n.k. Kwa hiyo aya "usitutie majaribuni" inaweza kumaanisha, "Tafadhali usinitelekeze kwa sababu peke yangu nitaserereka dhambini, au kubaki katika dhambi ambako nilishaserereka" au "ikiwa unanitahini, usiniache peke yangu wala kuniruhusu kubakia humo kwa muda mrefu kwa maana naogopa kudumbukia dhambini."

Wakati fulani Mungu anaruhusu au kukuweka katika mahali mahususi ili kukusaidia kuelewa moyo wako na hali yako ya kiroho, kufumbua macho yako kuona jinsi ulivyo na kile unachohitaji. Biblia inasema kwamba wewe "hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka,

na maskini, na kipofu, na uchi" (Ufu. 3:17). Unapojua kuwa wewe ni mgonjwa, unakwenda kwa dakitari, lakini unawezaje kushughulikia jambo ambalo hulifahamu?

Tunapoona vile tulivyo, tunagundua jinsi tulivyo wenye dhambi na kujua kuwa tunamhitaji Yesu. "Wanaoishi karibu kabisa na Yesu wanatambua kwa uwazi zaidi udhaifu na hali ya dhambi ya mwanadamu, na tumaini lao pekee linapatikana katika haki ya Mwokozi aliyesulubiwa na aliyefufuka" (*Pambano Kuu,* uk. 389, 390).

Mungu alimpa jaribio Mfalme Hezekia (2 Nyakati 32:31). Mithali 17:3 inasema kwamba, Mungu huijaribu mioyo. Daudi aliomba, "Ee Bwana, unijaribu na kunipima" (Zab. 26:2). Petro anasema kwamba majaribio makali wakati mwingine yanalenga kututahini (1 Petro 4:12).

"Kuziona dhambi zetu kunatusukuma Kwake Yeye anayeweza kusamehe; wakati nafsi, inapotambua unyonge wake, inapomwendea Yesu, atajidhihirisha katika uweza" (*Steps to Christ,* uk. 65).

Kwa hiyo, "Adui yetu mkuu anatafuta daima kuiweka nafsi inayotaabika mbali na Mungu" (*Prayer*, uk. 270). Anajua kwamba tukitengwa mbali na Mungu, tutasererekea dhambini.

Katika sehemu ya mwisho ya Sala ya Bwana, Yesu anajaribu kuwekea mkazo siri ya nguvu na ushindi. Anasema kwamba tumaini letu pekee linapaswa kuwapo daima ndani ya Yesu na kuwa na Yesu ndani yetu, kutotengana kamwe na kutoachana kamwe. "Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu" (Kol. 1:27).

Peke yetu hatuna uwezo wa kubadilisha na kukuza moyo mpya. Lakini ahadi iko wazi na thabiti: "mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya" (2 Kor. 5:17).

Kwa hivyo unajiangaliaje ili kuona mahali ulipo katika safari yako ya kiroho? Yesu anasema tunaweza kujua kwa matunda yetu (Mt. 7:16).

Unawezaje kuzaa matunda? Kwa kuwa umeunganishwa daima pamoja na Yesu (Yohana 15:1–5) na kujazwa na Roho Wake (Gal. 5:22, 23).

“Kuikiri dini kunawaweka watu katika kanisa, lakini tabia na mwenendo unaonesha kama wanao uhusiano wa kudumu na Kristo” (*The Desire of Ages*, uk. 676). Ili uendelee kubaki ndani Yake, hauhitaji kufahamu jinsi anavyotenda; unachohitaji ni kumwamini tu. Anawaokoa wale wote wanaomjia Yeye (Ebr. 7:25).

“Ulinzi pekee dhidi ya uovu ni uwepo wa Yesu moyoni” (*The Desire of Ages*, uk. 324).

Mungu anakuita ili kuomba bila kukoma, kudumu kuliitia Jina la Bwana, kutembea pamoja Naye na katika utambuzi wa uwepo Wake daima na utegemezi kamili juu Yake na kutotengwa mbali Naye kamwe. Hiyo ndiyo nguvu yako pekee. Na anaahidi kwamba mkimkaribia Mungu, “Naye atawakaribia ninyi” (Yakobo 4:8).

Hebu Tuombe Pamoja

**Muda wa Maombi (Dakika 30–45)**

*Vikundi vyote vya maombi vina njia tofauti za kuomba pamoja. Tunawahimiza kutumia dakika 30-45 zinazofuata katika maombi ya pamoja, kwa njia yo yote ambayo Roho Mtakatifu anaongoza. Tunahimiza maombi mafupi ya wazi (sentensi 1-3). Hii inaruhusu watu wengi zaidi kuomba mara nyingi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya kuomba kupitia Maandiko kulingana na mada. Unaweza kuomba kupitia aya nyingine pia na kujumuisha masomo mengine katika wakati wako wa maombi. Tazama Mwongozo wa Kiongozi na Maombi ya Maombi ya Kanisa Ulimwenguni kwa mawazo ya maombi.*

**Kuomba Sawasawa na Neno la Mungu—Yakobo 1:13.**

*“Maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu mtu.”*

**"Mungu Hawezi Kujaribiwa na Uovu"**

*Baba, tunakushukuru kwa kumtuma Yesu kuupinga na kuushinda uovu kwa niaba yetu. Kwako hakuna giza hata kidogo, ila wema na nuru. Tunajua kwamba tayari umeshaishinda dhambi na mauti na kwamba unatubadilisha ili tufanane na Wewe. Yafanye macho yetu kukitwa kwako!*

**"Wala Yeye Mwenyewe Hamjaribu Mtu"**

*Bwana, tafadhali usituruhusu tubaki katika majaribu ambayo yanaweza kututenga mbali nawe. Tufundishe kuzikimbia tamaa za ubinafsi zinazotushawishi na kuelekeza macho yetu kwenye tabia Yako isiyo na doa. Tuwezeshe kuchukia kile unachokichukia na kupenda kile unachokipenda.*

**Mapendekezo ya Maombi Zaidi**

**Shukrani na Sifa:** Shukuruni kwa baraka mahususi na Msifuni Mungu kwa wema Wake.

**Kuungama:** Tumia dakika chache kwa ajili ya maungamo binafsi na umshukuru Mungu kwa msamaha Wake.

**Uongozi:** Mwombe Mungu akupatie hekima kwa changamoto na maamuzi ya sasa.

**Kanisa Letu:** Ombea mahitaji ya kanisa katika ngazi ya majimbo na kanisa la ulimwengu (tazama karatasi nyingine yenye mahitaji).

**Mahitaji ya Eneo Mahalia:** Ombea mahitaji ya sasa ya washiriki wa kanisa, familia na majirani.

**Sikiliza na Uitike:** Tumia muda kuisikiliza sauti ya Mungu na kuitikia kwa sifa na nyimbo.

**Mapendekezo ya Nyimbo**

- Namwandama Bwana (Vk. 336 & Vd. 128)
- Ni Wako Bwana (Vk. 159 & Vd. 144)